TFDA/ADDO/…….

WIZARA YA AFYA NA USTAWI WA JAMII

# MAMLAKA YA CHAKULA NA DAWA

# MWONGOZO WA UWEZESHAJI MAFUNZO KWA WATOA DAWA KATIKA MADUKA YA DAWA MUHIMU

**MODULI 1- 5**

**2008**

**S. L. P. 77150, EPI Mabibo, Off Mandela Road, Dar es Salaam, Tel: +255-22-2450512/2450751/ 2452108, Fax: +255-22-2450793, Website: www.tfda.or.tz, Email: info@tfda**

Kitabu hiki kimetayarishwa na Mamlaka ya Chakula na Dawa  (TFDA) kwa ushirikiano na shirika lisilo la kiserikali la Management Sciences for Health(MSH).

**YALIYOMO** **UKURASA**


**VIFUPISHO**......................................................................................................iv
**DIBAJI** ...............................................................................................................v
**UTANGULIZI** ...................................................................................................... 1
**MTAZAMO WA MAFUNZO *(COURSE OVERVIEW)*** ................................................... 2
**NAMNA YA KUTUMIA KITABU CHA MWONGOZO WA MWEZESHAJI**......................... 4
**1.0MODULI YA KWANZA: SHERIA NA KANUNI ZA MADUKA YA DAWA MUHIMU NA MAADILI YA MTOA DAWA**.............................................. 6
1.1 Sura (*unit*) ya kwanza: Sheria na kanuni za uendeshaji wa DLDM ......................6
1.2 Sura ya pili: Maadili na taratibu za kufuatwa na mtoa dawa wa DLDM...............9
**2.0 MODULI YA PILI: UBORA, UTOAJI NA MATUMIZI SAHIHI YA DAWA** ............ 12
2.1 Sura ya kwanza: Ufafanuzi wa misamiati na maneno muhimu..........................12
2.2 Sura ya pili: Ubora na utunzaji dawa ...............................................................14
2.3 Sura ya tatu: Matumizi sahihi na njia za kuingiza dawa mwilini .......................16
2.4 Sura ya nne: Taratibu na hatua za utoaji wa dawa ...........................................18
2.5 Sura ya tano: Uandikaji na utunzaji wa kumbukumbu....................................20
**3.0 MODULI YA TATU: MAGONJWA YANAYOTOKEA MARA KWA MARA KATIKA JAMII** ...................................................................... 23
3.1 Sura ya kwanza: Malaria.................................................................................23
3.2 Sura ya pili: Magonjwa ya njia ya hewa (respiratory infections)....................25
3.3 Sura ya tatu: Magonjwa ya mfumo wa njia ya chakula ....................................30
3.4 Sura ya nne: Magonjwa ya minyoo...................................................................41
3.5 Sura ya tano: Magonjwa ya ngozi ....................................................................44
3.6 Sura ya sita: Magonjwa ya sikio na macho......................................................51
3.7 Sura ya saba: Shinikizo la juu la damu *(hypertension)* .....................................53
3.8 Sura ya nane: Maumivu na uvimbejoto (pain and inflamation)..........................54
3.9 Sura ya tisa: Mshituko wa anafilaksia (anaphylactic shock).............................55
**4.0 MODULI YA NNE: AFYA YA UZAZI** ............................................................ 57
4.1 Sura ya kwanza: Uzazi wa mpango ..................................................................57
4.2 Sura la pili: Magonjwa yaenezwayo kwa njia ya kujamiana ..............................60
4.3 Sura ya tatu: Virusi vya UKIMWI na UKIMWI ..................................................62
**5.0 MODULI YA TANO: STADI ZA MAWASILIANO** ............................................... 65
5.1 Sura ya kwanza: Kujenga na kudumisha uhusiano bora katika DLDM.............65
5.2 Sura ya pili: Elimu ya afya kwa mteja .............................................................67
5.3 Sura ya tatu: Ushauri nasaha katika dldm .....................................................69
**TATHMINI YA MAFUNZO** ................................................................................ 72
**Viambatanisho** ............................................................................................... 73

**VIFUPISHO**

| | |
|---|---|
| ALu | Artemisinin/ Lumefantrine |
| DLDB | Duka la Dawa Baridi |
| DLDM | Duka la Dawa Muhimu |
| GIT | Gastro Intestinal Tract |
| IPT | Intermittent Presumptive Treatment |
| MoHSW | Ministry of Health and Social Welfare |
| MSH | Management Sciences for Health |
| NSAID's | Non-Steroidal Anti-Inflammatory Drugs |
| ORS | Oral Rehaydration Salt |
| OTC | Over the Counter Drugs |
| SP | Sulfadoxine/Pyrimethamine |
| TFDA | Tanzania Food and Drugs Authority |
| VVU | Virusi vya Ukimwi |
| WAUJ | Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii |
| WHO | World Health Organisation |

**DIBAJI**

Serikali kupitia Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii inatambua umuhimu wa kushirikiana na sekta binafsi ikiwa ni pamoja na wafanyabiashara wa dawa, ili kuboresha afya ya jamii. Hivyo katika kutimiza azma hiyo, serikali imeanzisha Mpango wa Maduka ya Dawa Muhimu (DLDM). Moja ya kipengele muhimu cha kufanikisha mpango huu ni kutoa mafunzo kwa Watoa Dawa.

Mwongozo wa Uwezeshaji Mafunzo kwa Watoa Dawa DLDM ni moja ya nyenzo zilizotayarishwa na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa madhumuni ya kufanikisha mafunzo ya Mtoa Dawa. Aidha, mwongozo huu unalenga wawezeshaji na matumizi yake yanaenda sanjari na Kitabu cha Mafunzo ya Mtoa Dawa katika DLDM. Utumiaji kamilifu wa mwongozo huu utachangia kupunguza tofauti za ubora wa uwezeshaji hususan mafunzo yanapoendeshwa na wawezeshaji wenye uzoefu unaotofautiana na katika mazingira tofauti.

Mwongozo huu ni muhimu kwa kuzingatia kwamba wengi wa washiriki wa mafunzo haya ni watu wazima ambao mahitaji yao ya mafunzo yanahitaji mbinu shirikishi na zinazozingatia mahitaji ya kipekee kwa watu wazima. Hivyo, mwongozo huu ukitumika vema utachangia kufanikisha mafunzo ya Mtoa Dawa katika DLDM.

Ni matumaini yangu kwamba watakaotumia mwongozo huu wataufurahia na kufuata maelekezo ambayo pengine ni mapya kwao. Pia mwongozo uwe chachu katika kupata mbinu mpya za uwezeshaji ambazo zitakidhi mahitaji ya washiriki kadri yatakavyojitokeza kufuatia kusambazwa kwa Mpango huu nchi nzima.

**Mkurugenzi Mkuu,**
**Mamlaka ya Chakula na Dawa,TFDA**

## UTANGULIZI

Mnamo mwaka 2001 Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kupitia Mamlaka ya Chakula na Dawa ikishirikiana na shirika lisilo la kiserikali la *Management Sciences for Health (MSH)* iliendesha tathmini juu ya hali halisi ya utendaji katika sekta ya dawa nchini. Katika tathimini hiyo ilionyesha kwamba licha ya mambo mengine, Maduka ya Dawa Baridi yamesambaa karibu kila sehemu ya nchi hadi maeneo ya vijijini ambako ndiko sehemu kubwa ya watanzania wanaishi. Ilithibitika kwamba maduka hayo ni kimbilio la wananchi kwa ajili ya kupata huduma ya dawa baada ya kukosa dawa hizo katika vituo vya huduma ya afya vya umma. Tathmini hiyo pia ilibaini kuwepo kwa wafanyakazi wasio na sifa za kuuza dawa katika maduka hayo, kulingana na matakwa ya *Mwongozo wa Maduka ya Dawa Baridi wa mwaka 1998*.

Ilibainika kuwa, asilimia hamsini (50%) ya wafanyakazi wa maduka hayo walikuwa ni "wahudumu wa afya" asilimia kumi na sita (16%) walikuwa ni tabibu, asilimia kumi na tatu (13%) walikuwa ni Wauguzi Wakunga. Aidha, tathmini hiyo ilionyesha kuwa asilimia ishirini na moja (21%) ya wafanyakazi katika DLDB walikuwa hawana ufahamu au elimu yoyote kuhusu sayansi ya tiba au dawa.

Kutokana na tathimini hii Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii iliamua kufanya mabadiliko ya msingi katika uendeshaji wa Maduka ya Dawa Baridi (DLDB) nchini, hasa kwa kuzingatia kuboresha utaalam wa Watoa Dawa katika DLDB. Ndipo iliamuliwa kuwa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kupitia Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) ikishirikiana na *Management Sciences for Health (MSH)* iandae mafunzo maalum ambayo ni lazima ayafuzu mtu yoyote anayetaka kutambuliwa kama Mtoa Dawa kwenye Maduka ya Dawa Muhimu. Mafunzo haya yamelenga watoa dawa ambao ni kada zifuatazo: Mhudumu wa Afya (Uuguzi), Afisa Muuguzi, Muuguzi Mkunga, Muuguzi Msaidizi, Tabibu, Tabibu Msaidizi, Fundi Dawa Sanifu, Fundi Dawa Sanifu Msaidizi.

Mafunzo haya yatachukua takriban wiki tano na yanalenga kumwezesha Mtoa Dawa kuweza kutekeleza majukumu yake ya msingi katika DLDM mathalani kutoa dawa kwa usahihi na katika hali itakayochangia matumizi bora ya dawa, na kwa kufuata maadili ya Mtoa Dawa.

Kozi hii imegawanyika katika moduli tano kama zifuatazo: (a) Sheria na Kanuni za Maduka ya Dawa Muhimu na Maadili ya Mtoa Dawa (b) Ubora, Utoaji na Matumizi sahihi ya Dawa, (c) Magonjwa Yatokeayo Mara kwa Mara katika Jamii (d) Afya ya Uzazi (e) Stadi za Mawasiliano.

Wanafunzi katika kozi hii wanatakiwa kuhudhuria masomo haya kwa asilimia mia, na kufaulu mitihani itakayotolewa kila baada ya moduli. Wanafunzi watakaofuzu watatunukiwa vyeti toka Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kupitia Mamalaka ya Chakula na Dawa. Wawezeshaji katika mafunzo haya wanatarajiwa kuwa Watalaamu wa Afya na stadi za mawasiliano ambao watawezesha kwa kutumia mbinu shirikishi za kufundishia watu wazima. Aidha, Vyuo vya Mafunzo ya Afya vya Kanda *(Zone Health Training Institutes)* vitatumika kuendesha mafunzo haya.

## MTAZAMO WA MAFUNZO *(COURSE OVERVIEW)*

### 1.0 Mwongozo wa Uwezeshaji wa Masomo ya Watoa Dawa

Kitabu hiki cha Mwongozo wa Uwezeshaji kimetayarishwa ili kuwaongoza Wawezeshaji wa mafunzo kwa Watoa Dawa wa Duka la Dawa Muhimu (DLDM) ili waweze kupata ujuzi na maarifa ya kumudu utekelezaji wa wajibu wao na hatimaye kuboresha huduma zinazotolewa.

Katika mafunzo haya inategemewa kwamba Watoa Dawa watawezeshwa:

- Kuelewa misingi ya utoaji sahihi wa dawa.
- Kufuata Kanuni za Uendeshaji wa DLDM na maadili ya Mtoa Dawa katika DLDM.
- Kuwa na ujuzi wa uandikaji na utunzaji wa kumbukumbu kwenye DLDM.
- Kuwa na uelewa wa magonjwa yatokeayo mara kwa mara katika jamii, dalili na tiba yake.
- Kufahamu madhara yatokanayo na matumizi ya dawa zinazotumika kutibu magonjwa hayo.
- Kutoa huduma bora kwa kuzingatia mawasiliano mazuri na wateja wa DLDM.

### 2.0 Mambo ya Kuzingatia Unapofundisha Watu Wazima

Ili kuweza kufikia malengo ya mafunzo haya, kwa kuzingatia kuwa wengi wa washiriki ni watu wazima ambao tayari wameshafanya kazi ya kutoa dawa kwenye vituo vya huduma ya afya ikiwemo DLDB, ni muhimu kwa wawezeshaji kutumia mbinu shirikishi za kufundishia watu wazima (*Adult learning and educational skills*). Mbinu hizi zitawafanya washiriki kuelewa mafunzo kwa urahisi na kupata ujuzi na maarifa yanayohitajika katika kuboresha huduma zitolewazo katika DLDM.

### *2.1. Mtu Mzima anavyojifunza*

Mtu mzima anajifunza kirahisi ikiwa:

- Wawezeshaji wa mafunzo wanajali mahitaji yake binafsi yahusuyo namna anavyojifunza (*learning style or needs*)
- Ana moyo wa kutaka kujua yanayofundishwa
- Anachojifunza atakitumia mara tu amalizapo mafunzo, pia anaona kwamba kitamsaidia kuboresha huduma anayoitoa.
- Anawajibika kuhusu kujifunza.
- Yeye na wenzake wanapewa nafasi ya kupeana mawazo yatokanayo na uzoefu wa suala linalohusika.
- Mazingira ya ukufunzi wake yanamvutia na kumpa motisha ya kusoma.
- Anaona kwamba anaheshimiwa, anaaminika, anasikilizwa na pia anafanya maamuzi ya jinsi ya kujifunza.

### 3.0 Mambo Muhimu ya Kufanya Wakati wa Siku ya Kwanza ya Mafunzo

Wawezeshaji wafike darasani angalau saa moja kabla ya kuanza mafunzo ili aweze kufanya yafuatayo:

a) Waangalie mpangilio wa darasa na vifaa vya kufundishia.
b) Wakaribishe washiriki kwa kuwasalimia na kujitambulisha.

c) Waombe washiriki kila mmoja ajitambulishe kwa kueleza anatoka wapi na anafanya kazi gani.

d) Gawia washiriki *“name tags”* ili waweze kuandika majina yao, na hakikisha unawataja kwa majina hayo.

e) Elezea mpangilio wa mafunzo, kama vile muda wa vipindi, muda wa chai, muda wa mapumziko na chakula na mambo mengine muhimu yanayotakiwa kuzingatiwa na washiriki.

f) Wape washiriki makabrasha ya kozi ikiwa ni pamoja na Kitabu cha Mwongozo wa Mtoa dawa wa DLDM na ratiba ya mafunzo.

g) Waeleze kuwa kutakuwa na mazoezi na mtihani kwa kila moduli ambapo kila mshiriki anapaswa kufaulu ili aweze kutunukiwa cheti *(Certificate)* cha Mtoa Dawa wa Duka la Dawa Muhimu.

h) Waongoze washiriki wachague Mwenyekiti wa mafunzo, viongozi wa madarasa na watunza muda kwa kila darasa.

## NAMNA YA KUTUMIA KITABU CHA MWONGOZO WA MWEZESHAJI

### 1. MWEZESHAJI AFANYE NINI

- Kusoma na kuelewa kwa ufasaha Kitabu cha Mafunzo ya Mtoa Dawa na Mwongozo wa Mwezeshaji
- Tayarisha andalio la kila somo *(lesson plan)* ikiwa ni pamoja na vifaa vya kufundishia

### 2. MBINU ZA UWEZESHAJI

- Chagua mbinu muafaka za ufundishaji kwa kuzingatia maudhui ya somo na mazingira ya ufundishaji
- Andaa mazoezi ya vitendo na vifaa husika, majadiliano katika vikundi, ilihali, igizo n.k.

### 3. MUDA WA MAFUNZO

- Ili kutoa uzito na uwiano sawa kwa sura ni muhimu kuzingatia muda uliopangwa kwa kila sura

### 4. UFUATILIAJI WA MAFUNZO

- Hakikisha kwamba washiriki wanakusikiliza, wapo makini na wanashiriki kikamilifu kwenye majadiliano na kazi za vikundi
- Tambua uwezo na ushiriki wa mshiriki mmoja mmoja na hasa wale wenye kasi ndogo ya kuelewa
- Badilisha mbinu za ufundishaji kulingana na uelewa wa washiriki
- Toa msaada kwa washiriki wenye kasi ndogo ya kuelewa
- Toa mazoezi kila mwisho wa somo na watake wawasilishe kabla ya kuanza somo nyingine

### 5. TATHMINI YA MAFUNZO

- Toa mitihani ya majaribio katikati ya moduli
- Toa mtihani wa mwisho wa moduli
- Andaa maswali na majibu kwa ajili ya mtihani wa mwisho wa mafunzo
- Watake washiriki watathmini uendeshaji wa mafunzo kwa kujaza fomu maalum kila mwisho wa moduli

# Moduli ya Kwanza

## 1.0 MODULI YA KWANZA: SHERIA NA KANUNI ZA MADUKA YA DAWA MUHIMU NA MAADILI YA MTOA DAWA

**Muda wa moduli:** **Saa 11:45**

**Utangulizi wa Moduli**

**Utaratibu wa uwezeshaji (*Task*):** **Dakika 25**

- **Tengeneza** mazingira mazuri ya kufundishia (dk. 5)
- **Elezea** utangulizi wa moduli (dk. 5)
- **Elezea** lengo la moduli (dk. 5)
- **Taja** sura zilizoko katika moduli (dk. 5)
- **Wafahamishe** jinsi watakavyotathminiwa (dk. 5)

### 1.1 SURA (*UNIT*) YA KWANZA: SHERIA NA KANUNI ZA UENDESHAJI WA DLDM

**Muda:** **Saa 6.30**

**Malengo Mahususi ya Sura**

Ifikapo mwisho wa sura hii washiriki wataweza kueleza:

- Maana ya sheria, kanuni na mwongozo katika uanzishwaji na uendeshaji wa DLDM
- Vifungu vya sheria na Kanuni za DLDM
- Vigezo na viwango *(standards)* muhimu vya DLDM
- Kuwepo kwa Duka la Dawa la Jumla Lenye Mipaka
- Makosa na adhabu zinazohusiana na ukiukwaji wa kanuni za DLDM
- Taratibu za rufaa

**Baadhi ya mbinu za kufundishia:**

- Mhadhara wa majadiliano (*lecture-discussion*)
- Bunga bongo
- Majadiliano kwa vikundi
- Igizo
- Ilhali

**Vifaa vya Kufundishia na Kujifunza:**

- Chati pindu (flip chart) (*Flipchart*)
- Gundi ya karatasi
- “Marker pen”
- Ubao na chaki
- Bango la ngazi ya uendeshaji wa DLDM
- Vitabu vya Kiada (Kitabu cha Mafunzo kwa Watoa Dawa, Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi ya mwaka 2003 na Kanuni za Maduka ya Dawa Muhimu)

**Utaratibu wa uwezeshaji 1 (Matatizo ya Maduka ya Dawa Baridi na Misamiati): Saa 1.00**

- **Tengeneza** mazingira mazuri ya kufundishia (*Climate Setting*): (dk. 5)
- **Onesha** (display) malengo ya sura yaliyoandikwa kwenye Chati pindu (flip chart) (dk.5)
- **Fafanua** malengo ya sura (dk. 5)
- **Waambie** washiriki wasome na wajadili ilihali iliyo katika kiambatanisho Na. 1 (angalia sehemu ya viambatanisho) kuhusu makosa na adhabu za uvunjaji wa kanuni za DLDM. Ilihali ipo pia kwenye kitabu cha mwanafunzi.
- Kanuni za kanuni wabunge bongo matatizo ya undeshaji katika Maduka ya Dawa Baridi (dk. 10 )
- **Toa** majumuisho ya matatizo ya undeshaji katika Maduka ya Dawa Baridi za kuwepo kwa kulinganisha na majibu yao (dk. 5)
- **Toa** sababu za kuanzishwa kwa DLDM (dk. 5)
- **Fafanua/eleza** maana ya istilahi za kisheria zinazotumika (dk. 25)

**Utaratibu wa uwezeshaji 2 (uanzishaji wa DLDM): Saa 2**

- **Eleza** mfumo wa uanzishaji wa DLDM kama ilivyoelezwa katika Kitabu cha Mtoa Dawa (dk. 60)
- **Uliza** washiriki maswali na toa maelezo kuhusu majibu sahihi (dk. 15)
- **Elekeza** washiriki wafanye igizo juu ya taratibu za uanzishaji wa DLDM kama lilivyoainishwa katika **kiambatanisho 3** (dk. 45)

**Utaratibu wa uwezeshaji 3 (udhibiti na ukaguzi): Saa 1**

- **Eleza** Udhibiti na ukaguzi wa DLDM ukiainisha ngazi mbalimbali zinazohusika (dk. 30)
- **Eleza** taratibu za kuendesha ukaguzi na ufuatiliaji (dk. 15)
- **Uliza** washiriki maswali na toa maeleezo kuhusu majibu sahihi (dk. 15)

**Utaratibu wa uwezeshaji 4 (vigezo vya DLDM): Saa 1:30**

- **Gawa** washiriki katika makundi ya watu 5-7 ili wajadili vigezo na viwango (standards) muhimu vya DLDM kuhusiana na Mtoa Dawa, mmiliki na jengo (dk. 5)
- **Ruhusu** majadiliano katika vikundi (dk. 15)
- **Ruhusu** kila kikundi wawasilishe mambo waliojadiliana kwa muda wa dk. 5 (dk. 40)
- **Linganisha** mambo waliowasilisha na maelezo yaliyomo kwenye kitabu cha mafunzo (dk. 25)

**Utaratibu wa uwezeshaji 5: Saa 1**

- **Eleza** mahitaji muhimu katika uendeshaji wa DLDM (dk. 10)
- **Eleza** umuhimu wa mafunzo endelevu *(continuing education)* (dk. 5)
- **Eleza** umuhimu wa kuwa na mkataba wa kazi (dk. 10)
- **Eleza** kuhusu duka la dawa la jumla lenye mipaka (dk. 5)

- **Waambie** washiriki wasome maelezo ya ilihali kuhusu makosa yanayohusu ukikwaji wa Kanuni za DLDM yaliyo katika **kiambatanisho 1** na waulize maswali (dk 15)
- **Eleza** makosa na adhabu zinazohusiana na ukiukwaji wa kanuni za DLDM (dk. 15)
- **Elezea** taratibu za rufaa kuhusiana na uendeshaji wa DLDM (dk. 5)
- **Hitimisha** kwa maswali na majibu (dk. 10)

## 1.2 SURA YA PILI: MAADILI NA TARATIBU ZA KUFUATWA NA MTOA DAWA WA DLDM

**Muda: Saa 5:15**

### Malengo mahususi

Ifikapo mwisho wa sura hii washiriki wataweza:

- Kuelezea maadili ya Mtoa Dawa kwenye DLDM
- Kuelezea taratibu za kufuatwa katika huduma za DLDM
- Kuainisha haki za mteja

**Baadhi ya Mbinu za Kufundishia na Kujifunza:**

- Mhadhara kwa majadiliano
- Bunga bongo
- Majadiliano katika vikundi
- Ilihali

**Vifaa vya Kufundishia:**

- Kitabu cha Mafunzo kwa Watoa Dawa
- Chati pindu (flip chart)
- Gundi ya karatasi
- *Marker pens*
- Ubao na chaki
- Kanuni za Maduka ya Dawa Muhimu

**Utaratibu wa uwezeshaji 1: Saa 2.10**

- **Tengeneza** mazingira mazuri ya kufundishia *(Climate Setting)* (dk. 5)
- **Onesha** (display) malengo ya sura yaliyoandikwa kwenye Chati pindu (flip chart)(dk.2)
- **Fafanua** malengo ya sura (dk. 5)
- **Toa** utangulizi wa sura (dk 8)
- **Gawa** washiriki katika makundi ya watu 5-7 ili wajadiliane ilihali iliyo katika **kiambatanisho 2** kuhusu maadili ya Mtoa Dawa Kwenye DLDM. (dk. 5)
- **Ruhusu** majadiliano katika vikundi (dk. 15)
- **Ruhusu** kila kikundi kiwasilishe mambo waliojadiliana kwa muda wa dk. 5 (dk. 40)
- **Linganisha** mambo waliowasilisha na maelezo yaliyomo kwenye kitabu cha mafunzo kwa kutoa mifano (dk.40)
- **Hitimisha** kwa maswali na majibu (dk. 10)

**Utaratibu wa uwezeshaji 2: Saa 2:30**

- **Elezea** misingi ya utoaji huduma katika DLDM (dk. 45)
- **Gawa** washiriki katika makundi ya watu 5-6 ili waorodheshe haki za mteja (dk. 3)
- **Ruhusu** majadiliano katika vikundi (dk. 15)
- **Ruhusu** kila kikundi kiwasilishe mambo waliojadiliana kwa muda wa dk. 5 (dk. 40)
- **Linganisha** mambo waliowasilisha na maelezo yaliyomo kwenye kitabu cha mafunzo kwa kutoa mifano (dk.40)
- **Hitimisha** kwa maswali na majibu (dk. 5)

**Kuhitimisha moduli**

**Utaratibu wa uwezeshaji: dk 35**

- **Uliza** eneo ambalo linahitaji ufafanuzi katika sura zote (dk 5)
- **Fanya** majumuisho ya mambo ya msingi kwa kila sura (dk 10)
- **Fanya** tathmini moduli kwa kuwataka washiriki wajaze dodoso la tathmini (dk 20)

# Moduli ya Pili

## 2.0 MODULI YA PILI: UBORA, UTOAJI NA MATUMIZI SAHIHI YA DAWA

**Muda wa Moduli** **Saa 22**

**Utangulizi wa Moduli**

**Utaratibu wa uwezeshaji (*Task*):** **Dakika 25**

- **Tengeneza** mazingira mazuri ya kufundishia (dk. 5)
- **Elezea** utangulizi wa moduli (dk. 5)
- **Elezea** lengo la moduli (dk. 5)
- **Taja** sura zilizoko katika moduli (dk. 5)
- **Wafahamishe** jinsi watakavyotathminiwa (dk. 5)

### 2.1 SURA YA KWANZA: UFAFANUZI WA MISAMIATI NA MANENO MUHIMU

**Muda:** **Saa 2**

**Lengo Mahususi**

Ifikapo mwisho wa sura hii Mtoa Dawa ataweza kufafanua misamiati na vipengele muhimu vinavyohusiana na utoaji dawa.

**Baadhi ya Mbinu za Kufundishia na Kujifunza:**

- Mhadhara kwa majadiliano
- Bunga bongo
- Zoezi kwa vitendo

**Vifaa vya Kufundishia:**

- Kitabu cha Mafunzo ya Watoa Dawa
- Gundi ya karatasi
- *Marker pens*
- Ubao na chaki
- Sampuli za dawa zenye majina ya kibiashara na ya asili
- Sampuli ya cheti cha dawa cha daktari
- Picha mnato
- Projekta

**Utaratibu wa uwezeshaji:**

- **Tengeneza** Mazingira Mazuri ya Kufundishia *(Climate Setting)* Dakika 5
- **Soma** malengo ya somo na toa ufafanuzi (dk 5)

- **Elezea** maana ya misamiati na maneno kama yalivyoanishwa katika kitabu cha mwanafunzi (dk 80)
- **Onesha** sampuli za dawa na hakikisha washiriki wote wanaona:
    - Maumbo tofauti ya dawa
    - Majina ya dawa ya asili na ya kibiashara
    - Tarehe za utengenezaji na tarehe ya kuisha muda wa matumizi ya dawa (dk 20)
- **Hitimisha** kwa maswali na majibu ili kuhakikisha kama wameelewa maana ya Maneno, Misamiati na Vipengele Muhimu (dk. 10)

## 2.2 SURA YA PILI: UBORA NA UTUNZAJI DAWA

**Muda: Saa 3**

### Malengo Mahususi

Ifikapo mwisho wa sura hii washiriki wataweza kueleza:

- Viashiria vya ubora wa dawa
- Sifa za dawa zilizopoteza ubora
- Sababu za dawa kupoteza ubora
- Majukumu ya Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) katika kuhakiki ubora wa dawa
- Majukumu ya Mtoa Dawa katika kuhakikisha kuwa dawa ni bora

**Baadhi ya Mbinu za Kufundishia na Kujifunza:**

- Mhadhara kwa majadiliano
- Bunga bongo
- majadiliano kwa vikundi
- Mazoezi kwa vitendo

**Vifaa vya Kufundishia:**

- Kitabu cha Mafunzo ya Watoa Dawa
- Chati pindu (flip chart)
- Gundi ya karatasi
- *Marker pen*
- Ubao na chaki
- Sampuli za dawa zenye majina ya kibiashara na ya asili
- Sampuli za dawa bora na zisizo bora

**Utaratibu wa uwezeshaji: Saa 3:00**

- **Kutengeneza** Mazingira Mazuri ya Kufundishia *(Climate Setting)* (dk. 5)
- **Eleza** malengo ya somo (dk 10)
- **Gawa** washiriki katika makundi ya watu watano watano (dk. 5)
- **Ruhusu** majadiliano katika vikundi (dk. 15)
  - Ishara ya dawa zenye ubora
  - Ishara za dawa zilizopoteza ubora
  - Sababu za dawa kupoteza ubora wake
- **Ruhusu** kila kikundi wawasilishe mambo waliojadiliana (dk. 40)
- **Linganisha** mambo waliyowasilisha na maelezo yaliyomo kwenye Kitabu cha Mafunzo ya Watoa Dawa (dk.45)
- **Elezea** majukumu ya Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) katika kuhakikisha ubora wa dawa (dk 25)

- **Waambie** washiriki wabunge bongo kuhusu majukumu yao katika kuhakikisha ubora wa dawa (hakikisha unatoa majumuisho) (dk. 25)
- **Hitimisha** kwa maswali na majibu (dk. 10)

## 2.3 SURA YA TATU: MATUMIZI SAHIHI NA NJIA ZA KUINGIZA DAWA MWILINI

**Muda: Saa 2.40**

### Malengo mahususi

Ifikapo mwisho wa sura hii washiriki wataweza kueleza:

- Maana ya matumizi sahihi na yasiyo sahihi ya dawa
- Sababu zinazochangia matumizi ya dawa yasiyo sahihi
- Athari za matumizi ya dawa yasiyo sahihi
- Wajibu wa mtoa dawa katika kuhakikisha wagonjwa wanatumia dawa kwa usahihi
- Njia kuu za kuingiza dawa mwilini

**Baadhi ya Mbinu za Kufundishia na Kujifunza:**

- Mhadhara kwa majadiliano
- Bunga bongo
- Majadiliano katika vikundi

**Vifaa vya Kufundishia:**

- Kitabu cha Mafunzo kwa Watoa Dawa
- Chati pindu (flip chart)
- Gundi ya karatasi
- *Marker pen*
- Ubao na chaki
- Sampuli za dawa kwa ajili kuelezea njia za kuingiza dawa mwilini

**Utaratibu wa uwezeshaji: Saa 2.40**

- **Kutengeneza** Mazingira Mazuri ya Kufundishia *(Climate Setting)* (dk. 5)
- **Elezea** matumizi sahihi ya dawa (dk. 5)
- **Elezea** matumizi yasiyo sahihi ya dawa (dk. 20)
- **Gawa** washiriki katika makundi ya watu 5-7 (dk. 5)
- **Ruhusu** majadiliano katika vikundi (dk. 15);
    - sababu zinazochangia matumizi yasiyo sahihi ya dawa
    - sababu zinazomfanya mtoa dawa kuchangia matumizi yasiyo sahihi ya dawa
- **Ruhusu** kila kikundi kiwasilishe mambo waliyojadiliana kwa muda wa dk. 5 (dk. 40)
- **Linganisha** mambo waliyowasilisha na maelezo yaliyomo kwenye kitabu cha mafunzo (dk.15)
- **Waambie** washiriki wabunge bongo juu ya athari za matumizi yasiyo sahihi ya dawa (dk. 15)

- **Elezea** wajibu wa mtoa dawa katika kuhakikisha wagonjwa wanatumia dawa kwa usahihi (dk. 10)
- **Elezea** njia kuu tano (5) za kuingiza dawa mwilini (dk. 10)
- **Elezea** faida na upungufu wa kila njia ya kuingiza dawa mwilini (dk. 10)
- **Hitimisha** kwa kuuliza maswali ili kuhakikisha kama wamelewa matumizi sahihi na njia za kuingiza dawa mwilini (dk.10)

## 2.4 SURA YA NNE: TARATIBU NA HATUA ZA UTOAJI WA DAWA

**Muda: Saa 8:00**

**Malengo Mahususi**
Ifikapo mwisho wa sura hii washiriki wataweza kueleza:

- Utaratibu mzuri wa utoaji dawa
- Vipengele muhimu vya cheti cha daktari cha dawa
- Hatua muhimu za utoaji wa dawa za cheti
- Taratibu zinazotakiwa kufuatwa katika utoaji wa dawa zisizohitaji cheti (OTC)
- Hatua za kufuata wakati wa kuchanganya dawa za unga na maji

**Baadhi ya Mbinu za Kufundishia na Kujifunza:**

- Mhadhara kwa majadiliano
- Bunga bongo
- Majadiliano katika vikundi
- Igizo
- Mazoezi kwa vitendo

**Vifaa vya Kufundishia:**

- Kitabu cha Mafunzo kwa Watoa Dawa
- Chati pindu (flip chart)
- Gundi ya karatasi
- *Marker pens*
- Ubao na chaki
- Kalamu
- Sampuli ya dawa aina ya ORS (kwa ajili ya kuonyesha jinsi ya kuichanganya
- Maji safi na salama
- Sampuli ya vyeti vya dawa vya mganga vilivyoandikwa sahihi na vyenye mapungufu

**Utaratibu wa uwezeshaji:**

- **Tengeneza** Mazingira Mazuri ya Kufundishia *(Climate Setting)* (dk. 5)
- **Eleza** malengo ya somo (dk. 5)
- **Eleza** mazingira ya kutolea dawa (dk. 60)
- **Eleza** vipengele muhimu vya cheti sahihi cha dawa (dk. 20)
- **Eleza** maana na vifupisho mbalimbali vinavyotumika kuandika cheti cha dawa (dk. 30)
- **Gawa** washiriki katika vikundi vya watu 5-7 (dk 5)
- **Toa** zoezi la kutofautisha vyeti sahihi na visivyo sahihi (dk 10)
- **Ruhusu** vikundi kuwasilisha majibu yao kwa kundi kubwa ( dk 40)
- **Fanya** majumuisho kwa kusisitiza mambo muhimu kuhusu cheti sahihi (dk 10)

- **Toa** igizo kuhusu hatua za utoaji wa dawa kulingana na maelezo yaliyo katika **kiambatanisho namba 4** (dk 20)
- **Eleza** taratibu zinazotakiwa kufuatwa katika utoaji wa dawa za cheti (dk. 40)
- **Eleza** aina ya kumbukumbu zinazotakiwa kuwekwa (dk 60)
- **Eleza** taarifa muhimu za dawa kwa wagonjwa (dk 60)
- **Eleza** taratibu zinazotakiwa kufuatwa katika utoaji wa dawa zisizohitaji cheti (dk 30)
- **Toa** zoezi la vitendo juu ya hatua za utoaji wa dawa za cheti (dk 15)
- **Jumuisha** kwa kusisitiza hatua muhimu za utoaji dawa za cheti (dk 15)
- **Eleza** hatua za kufuata wakati wa kuchanganya dawa za unga na maji (dk 30)
    - washiriki wabungue bongo kuhusu dawa zinazotakiwa kuchanganywa na maji
    - toa maelezo kuhusu uchanganyaji wa dawa
    - Eleza jinsi ya kuchanganya dawa ya ORS
- **Onesha** jinsi ya kuchanganya dawa ya ORS *(demonstration)* (dk 15)
- **Hitimisha** kwa maswali na majibu (dk 10)

## 2.5 SURA YA TANO: UANDIKAJI NA UTUNZAJI WA KUMBUKUMBU

**Muda: Saa 6:00**

**Malengo Mahususi**

Ifikapo mwisho wa sura hii washiriki wataweza:

- Kutaja nyaraka mbalimbali za usimamizi katika Duka la Dawa Muhimu
- Kutaja manufaa ya ujazaji na utunzaji wa nyaraka mbalimbali katika DLDM
- Kujaza nyaraka mbalimbali za usimamizi katika DLDM

**Baadhi ya Mbinu za Kufundishia na Kujifunza:**

- Mhadhara kwa majadiliano
- Mazoezi kwa vitendo

**Vifaa vya Kufundishia:**

- Kitabu cha Mafunzo kwa Watoa Dawa
- Rejista na leja ya dawa
- *Bin Card*
- Fomu ya kutolea taarifa ya ukaguzi
- Fomu ya kutolea taarifa kuhusu malalamiko kutoka kwa mgonjwa kuhusu madhara ya dawa
- Nakala ya nyaraka zilizojazwa kwa usahihi
- Chati pindu (flip chart)
- Gundi ya karatasi
- *Marker pens*
- Ubao na chaki

**Utaratibu wa uwezeshaji:**

- **Tengeneza** Mazingira Mazuri ya Kufundishia *(Climate Setting)* dk 5
- **Eleza** malengo ya somo (dk 5)
- **Wambie** washiriki wabunge bongo kuhusu umuhimu wa kuifadhi nyaraka na kumbukumbu (dk 10)
- **Elezea** umuhimu wa kuifadhi nyaraka na kumbukumbu kwa kulinganisha na maelezo ya washiriki wakati wa bunga bongo(dk.10)
- **Elezea** makundi ya kumbukumbu (dk. 40)
- **Onesha** vitabu mbalimbali vya kumbukumbu (dk. 5)
- **Gawa** nakala za baadhi ya kurasa ya vitabu vya kumbukumbu (dk. 5)
- **Elezea** kwa vitendo namna ya kujaza nyaraka mbalimbali (dk. 60)
- **Wape** washiriki mazoezi ya kujaza nyaraka kwa dk. 25 kila fomu (dk. 175)
  - Pitia kwa washiriki kuona wanavyojaza nyaraka
  - Waelekeze pale wanapokosea kujaza nyaraka
- **Toa** maelezo ya jumla kuhusu uandikaji na utunzaji wa kumbukumbu (dk. 5)

- **Hitimisha** : kwa kuwapa nafasi washiriki watoe maoni yao kuhusu matumizi na ujazaji wa hizi nyaraka, kabla na baada ya mafunzo (dk. 5)

**Kuhitimisha moduli**

**Utaratibu wa uwezeshaji: dk 35**

- **Uliza** eneo ambalo linahitaji ufafanuzi katika sura zote (dk 5)
- **Fanya** majumuisho ya mambo ya msingi kwa kila sura (dk 10)
- **Fanya** tathmini moduli kwa kuwataka washiriki wajaze dodoso la tathmini (dk 20)

# Moduli ya Tatu

## 3.0 MODULI YA TATU: MAGONJWA YANAYOTOKEA MARA KWA MARA KATIKA JAMII

**Muda wa Moduli: Saa 54**

**Utangulizi wa Moduli**

**Utaratibu wa uwezeshaji (*Task*): Dakika 25**

- **Tengeneza** mazingira mazuri ya kufundishia (dk. 5)
- **Elezea** utangulizi wa moduli (dk. 5)
- **Elezea** lengo la moduli (dk. 5)
- **Taja** sura zilizoko katika moduli (dk. 5)
- **Wafahamishe** jinsi watakavyotathminiwa (dk. 5)

### 3.1 SURA YA KWANZA: MALARIA

**Muda: Masaa - 5.20**

**Malengo Mahsusi**

Ifikapo mwisho wa sura hii washiriki wataweza kueleza:

- Umuhimu wa ugonjwa wa malaria na unavyoenezwa
- Kutambua dalili za Malaria na tiba yake
- Malaria wakati wa ujauzito
- Tiba ya Tahadhari kwa Vipindi *(Intermittent Presumptive Treatment (IPT)* kwa mjamzito
- Kinga ya malaria

**Baadhi ya Mbinu za Kufundishia na Kujifunza**

- Mhadhara kwa majadiliano
- Bunga bongo
- Majadiliano katika vikundi vidogo (watu 2-6)
- Majadiliano katika kikundi kikubwa *(plenary)*
- Mazoezi ya vitendo

**Vifaa vya Kufundishia**

- Kitabu cha Mafunzo kwa Watoa Dawa
- Chati pindu (flip chart)
- Gundi ya karatasi
- *Marker pen*
- Ubao na chaki
- Kalamu
- Dawa za kutibu Malaria na maumivu/homa (Alu, SP, Quinine, Paracetamol)

**Utaratibu wa uwezeshaji 1: Saa 3**

- **Tengeneza** Mazingira Mazuri ya Kufundishia (Climate Setting): (dk 5)
- **Eleza** malengo ya sura (dk 5)
- **Elezea** kuhusu Malaria na kwamba ni ugonjwa muhimu hapa nchini (dk 5)
- Tumia bunga bongo ili washiriki wataje dalili za malaria na hakikisha wanatofautisha dalili za malaria kali na isiyo kali (dk 25).
- **Uliza** washiriki wataje malengo ya kutibu malaria isiyo kali? Andika majibu yao bila kupinga na kisha toa majumuisho (dk 10)
- **Elezea** tiba ya malaria isiyo kali (Dawa ya ngazi ya kwanza)kwa kutumia mifano (dk 20)
- **Toa** zoezi kuhusu utoaji na utumiaji wa kozi ya ALu kwa wagonjwa waliofika katika DLDM kwa saa tofauti (dk 55)
- **Jumuisha** kwa kusisitiza utoaji na utumiaji wa kozi ya ALu (dk 10)
- **Uliza** washiriki wataje dawa ya ngazi ya pili katika kutibu malaria na hakikisha unatoa jibu sahihi (quinine) (dk 5)
- **Elezea** dawa ya Ngazi ya Pili ($2^{nd}$ line) katika kutibu malaria. Tumia jedwali la tiba kufuatana na umri na uzito kwa dawa ya Kwinini (Quinine 300mg) (dk 20)
- **Elezea** kuhusu kutibu homa kwa mgonjwa wa malaria. Tumia jedwali kuelezea utaratibu wa kutibu homa kwa kutumia paracetamol (dk 10)
- **Elezea** tiba kwa malaria kali (dk 10)

**Utaratibu wa uwezeshaji 2: Saa 2.20**

- **Elezea** malaria kwa wajawazito (dk. 5)
- **Elezea** madhara ya malaria wakati wa ujauzito ( dk. 5)
- **Wambie** washiriki wabunge bongo juu ya madhara yanayoweza kutokea kwenye mimba yenyewe (dk. 10)
- **Oanisha** majibu yao na yale yaliyomo kwenye kitabu cha mafunzo kwa watoa dawa (dk. 5)
- **Elezea** matibabu ya tahadhari kwa vipindi (Intermittent Presumptive Treatment (IPT) (dk. 20)
- **Elezea** hatua za kuchukua kwa mjamzito mwenye dalili za malaria (dk. 10)
- **Uliza** maswali kuhusu matumizi ya Alu kwa wajawazito wenye (dk. 20)
- **Wagawe** washiriki katika makundi ya watu 5 na wajadili kinga ya malaria (dk. 15)
- **Ruhusu** vikundi viwasilishe majadiliano yao kwenye kundi kubwa (plenary) na toa majumuisho ya majadiliano (dk. 40)
- **Hitimisha** kwa kuwauliza washiriki wataje mambo 2 wanayoyakumbuka kuhusu matibabu ya Malaria isiyo kali na matumizi Alu (dk. 10)

## 3.2 SURA YA PILI: MAGONJWA YA NJIA YA HEWA (RESPIRATORY INFECTIONS)

**Muda: saa 8**

**Malengo Mahsusi**

Ifikapo mwisho wa sura hili washiriki wataweza:

- Kufanunua mfumo wa njia ya hewa
- Kueleza dalili za magonjwa ya njia ya hewa
- Kutoa dawa sahihi kutibu magonjwa ya njia ya hewa
- Kutoa ushauri sahihi na rufaa kwa wateja stahili

### 3.2.1 MAGONJWA YA SEHEMU YA JUU YA MFUMO WA NJIA YA HEWA

### (i) MAFUA NA KIKOHOZI (COMMON COLD/COUGH)

**Muda: Saa 1**

**Baadhi ya Mbinu za Kufundishia na Kujifunza**

- Mhadhara kwa majadiliano
- Bunga bongo

**Vifaa vya Kufundishia**

- Kitabu cha Mafunzo kwa Watoa Dawa
- Mchoro wa mfumo wa njia ya hewa
- Chati pindu (flip chart)
- Gundi ya karatasi
- *Marker pen*
- Ubao na chaki
- Kalamu

**Utaratibu wa uwezeshaji 1: Saa 2:15**

- **Tengeneza** mazingira mazuri ya kufundishia *(Climate Setting)* Dakika 5
- **Eleza** malengo mahsusi ya sura (dk 5)
- **Eleza** utangulizi wa sura ya magonjwa ya njia ya hewa (respiratory tract infections) na tumia mchoro kutoa maelezo ya mfumo wa hewa (dk. 20)
- **Elezea** kuhusu maambukizi ya mafua (dk. 10)
- **Wambie** washiriki wabunge bongo juu ya dalili za Mafua na toa ufafanuzi (dk. 10)
- **Elezea** tiba ya Mafua (dk. 10)
- **Elezea** tahadhali kuhusu Tiba ya Mafua (dk. 15)
- **Elezea** ushauri kwa mgonjwa (dk. 15)
- **Hitimisha** kwa maswali na majibu (dk 10)

**Utaratibu wa uwezeshaji 2: dk 35**

- **Elezea** kuhusu maambukizi ya kikohozi (dk. 5)
- **Wambie** washiriki wabunge bongo juu ya dalili za kikohozi na toa ufafanuzi (dk. 10)
- **Elezea** tiba ya kikohozi (dk. 10)
- **Elezea** tahadhali kuhusu kikohozi (dk. 5)
- **Hitimisha** kwa maswali na majibu (dk 5)

**(ii) KOO JEKUNDU (MAFINDOFINDO)** *PHARYNGOTONSILLITITIS*

**Muda: Saa 1**

**Baadhi ya Mbinu za Kufundishia na Kujifunza:**

- Mhadhara kwa majadiliano
- Bunga bongo
- Maswali na majibu

**Vifaa vya Kufundishia:**

- Kitabu cha Mafunzo kwa Watoa Dawa
- Chati pindu (flip chart)
- Gundi ya karatasi
- *Markers*
- Ubao na chaki
- Kalamu

**Utaratibu wa uwezeshaji: saa 1**

- **Tengeneza** Mazingira Mazuri ya Kufundishia *(Climate Setting)* (dk 10)
- **Soma** malengo na uyafafanue (dk. 5)
- **Waulize** washiriki kama wamewahi kuugua au kumwona mgonjwa wa Koo jekundu na dalili zake (dk. 10)
- **Eleza** kuhusu dalili za ugonjwa wa Koo jekundu (dk. 10)
- **Ruhusu** washiriki kuuliza maswali (dk 5)
- **Eleza** kuhusu tiba ya Koo jekundu (dk. 15)
- **Hitimisha** kwa maswali na majibu ya washiriki (dk 5)

### (iii) BRONKITI (BRONCHITIS)

**Muda: - Saa 1.15**

**Baadhi ya Mbinu za Kufundishia na Kujifunza**

- Mhadhara kwa majadiliano
- Bunga bongo

**Vifaa vya Kufundishia**

- Kitabu cha Mafunzo kwa Watoa Dawa
- Chati pindu (flip chart)
- Gundi ya karatasi
- *Marker pen*
- Ubao na chaki

**Utaratibu wa Uwezeshaji:**

- **Tengeneza** mazingira mazuri ya kufundishia (dk 5)
- **Toa** maelezo kuhusu bronkiti na aina zake(dk 5)
- **waelekeze** washiriki wabunge bongo kuhusu dalili za bronkiti kali (dk 10)
- **Toa** majumuisho kwa kulinganisha na dalili zilizoainishwa katika Kitabu cha Mafunzo(dk 10)
- **Elezea** matibabu ya bronkiti kali(dk 10)
- **Elezea** Bronkiti sugu na dalili zake (dk. 15)
- **Elezea** Mambo muhimu ya kuzingatia kuhusu bronkiti (dk 10)
- **Hitimisha** kwa maswali na majibu (dk 10)

### 3.2.2 MAGONJWA YA SEHEMU YA CHINI YA MFUMO WA NJIA YA HEWA

**(i) NIMONIA** *(PNEUMONIA)*

**Muda: Saa 2**

**Baadhi ya Mbinu za Kufundishia na Kujifunza**

- Mhadhara kwa majadiliano
- Bunga bongo
- Majadiliano katika vikundi
- Mazoezi ya vitendo

**Vifaa vya Kufundishia**

- Kitabu cha Mafunzo kwa Watoa Dawa
- Kielelezo (Mchoro wa viungo vya njia ya hewa)
- Chati pindu (flip chart)
- Gundi ya karatasi
- *Markers*
- Ubao na chaki
- Kalamu

**Utaratibu wa uwezeshaji: Saa 2**

- **Tengeneza** Mazingira Mazuri ya Kufundishia: (dk 5)
- **Elezea** maana ya ugonjwa wa Nimonia *(pneumonia)* (dk. 5)
- **Elezea** njia za kueneza ugonjwa wa Nimonia (dk. 10)
- **Onesha** sehemu zinazohusika na ugonjwa wa Nimonia kwa kutumia kielelezo (mchoro wa mfumo wa njia ya hewa) (dk. 5)
- **Waambie** Washiriki wabunge bongo kwa kutaja dalili za ugonjwa wa nimonia (dk 20)
- **Toa** ufafanuzi pale waliposhindwa kutaja dalili muhimu za nimonia kama zilivyoainishwa kwenye mwongozo wa mtoa dawa (dk 15)
- **Uliza** maswali kuhusu njia za kueneza ugonjwa wa Nimonia na dalili zake (dk. 10)
- **Elezea** tiba ya Nimonia (dk. 15)
- **Toa** zoezi la ukokotoaji wa dozi na kozi ya dawa za nimonia (dk 20)
- **Elezea** mambo ya kukumbuka kabla ya kutoa dawa kwa mgonjwa wa Nimonia (dk. 10)
- **Hitimisha** kwa kuwauliza washiriki maswali kuhusu dalili na tiba ili kujua kama wameelewa somo (dk. 5)

### (iii) UGONJWA WA PUMU

**Muda: Saa 1:20**

**Baadhi ya Mbinu za Kufundishia na Kujifunza**

- Mhadhara kwa majadiliano
- Bunga bongo
- Zoezi kwa vitendo

**Vifaa vya Kufundishia:**

- Kitabu cha Mafunzo kwa Watoa Dawa
- Chati pindu (flip chart)
- Gundi ya karatasi
- *Marker pen*
- Ubao na chaki

**Utaratibu wa uwezeshaji: saa**

- **Tengeneza** Mazingira Mazuri ya Kufundishia (dk 5)
- **Elezea** kwa kifupi kuhusu Ugonjwa wa pumu (dk. 5)
- **Wambie** washiriki wabunge bongo juu ya dalili za Ugonjwa wa pumu (dk 10)
- **Elezea** mapungufu/ongezea dalili ambazo hawakutaja (dk. 5)
- **Elezea** tiba ya Pumu (dk. 10)
- **Toa** zoezi la ukokotoaji wa dozi na kozi ya dawa za pumu (dk 20)
- **Elezea** kuhusu maudhi ya dawa ya Pumu (dk. 10)
- **Elezea** ushauri kwa mgonjwa wa Pumu (dk. 5)
- **Elezea** kuhusu tahadhari kabla ya kutoa dawa za kutibu Pumu (dk. 5)
- **Hitimisha** kwa maswali na majibu kwa wanafunzi (dk 5)

## 3.3 SURA YA TATU: MAGONJWA YA MFUMO WA NJIA YA CHAKULA

**Muda: Saa 11:45**

**Malengo Mahsusi**
Ifikapo mwisho wa sura hii washiriki wataweza kueleza:

- Sehemu kuu za mfumo wa njia ya chakula
- Magonjwa ya mfumo wa njia ya chakula yanayojitokeza mara kwa mara na dalili zake
- Dawa sahihi za kutibu magonjwa ya mfumo wa njia ya chakula yanayojitokeza mara kwa mara na utoaji wa rufaa
- Njia za kuzuia magonjwa ya mfumo wa njia ya chakula yanayojitokeza mara kwa mara

### 3.3.1 MAGONJWA YA KUAMBUKIZA KATIKA MFUMO WA CHAKULA

#### (i) KUHARISHA

**Muda: Saa 3**

**Baadhi ya Mbinu za Kufundishia na Kujifunza**

- Mhadhara kwa majadiliano
- Bunga bongo
- Maswali na majibu
- Majadiliano katika vikundi
- Mazoezi kwa vitendo

**Vifaa vya Kufundishia:**

- Kitabu cha Mafunzo kwa Watoa Dawa
- Mchoro wa mfumo wa njia ya chakula
- Vielelezo - ORS
- Maji na kifaa cha kuchanganyia ORS
- Chati pindu (flip chart)
- Gundi ya karatasi
- *Marker pen*
- Ubao na chaki

**Utaratibu wa uwezeshaji:**

- **Tengeneza** Mazingira Mazuri ya Kufundishia (dk 5)
- **Soma** malengo ya somo na uyafafanue (dk. 5)
- **Waruhusu** washiriki kuuliza maswali (dk. 5)
- **Toa** utangulizi kuhusu mfumo wa njia ya chakula kwa kutumia mchoro (dk 10)

- **Wambie** washiriki wabunge bongo kuhusu maana ya ugonjwa wa kuharisha na jinsi unavyoenezwa (dk 10)
- Toa ufafanuzi kwa kuoanisha majibu yao na yale yaliyomo katika kitabu cha mwanafunzi (dk. 10)
- **Elezea** makundi/aina za kuharisha (dk. 5)
- **Wagawe** washiriki katika makundi ya watu 5-7 (dk. 5)
- **Waambie** wajadili dalili muhimu za ugonjwa wa kuharisha na kuandika majibu yao kwenye Chati pindu (flip chart)  (dk 10)
- **Ruhusu** kila kikundi kiwasilishe majibu yao kwenye kikundi kiwasilishe kwenye kikundi kikubwa na toa majumuisho (dk 40)
- **Elezea** tiba ya ugonjwa wa kuharisha (dk 10)
- **Elezea** matumizi bora ya maji ya chumvichumvi (ORS) (dk. 25)
- **Teua** washiriki wawili waoneshe jinsi ya kuchanganya ORS (dk 15)
- **Wakumbushe** washiriki kumtaadharisha mgonjwa wa kuharisha kutumia maji ya chumvichumvi ili aepuke kupatiwa maji kwa njia ya mshipa wa damu (dk. 5)
- **Waelekeze** washiriki mambo muhimu ya kumtaarifa mgonjwa wa kuharisha (dk. 10)
- **Hitimisha** kwa maswali na majibu (dk 10)

**(ii) KUHARISHA DAMU** *(DYSENTRY)*

**Muda: Saa - 2.15**

**Baadhi ya Mbinu za Kufundishia na Kujifunza**

- Mhadhara kwa majadiliano
- Bunga bongo
- Majadiliano katika vikundi
- Mazoezi ya vitendo

**Vifaa vya Kufundishia**

- Kitabu cha Mafunzo kwa Watoa Dawa
- Mchoro wa mfumo wa chakula
- Chati pindu (flip chart)
- Gundi ya karatasi
- *Marker pen*
- Ubao na chaki

**Utaratibu wa uwezeshaji**

- **Tengeneza** Mazingira Mazuri ya Kufundishia (dk. 5)
- **Soma** malengo ya somo na uyafafanue (dk. 5)
- **Elezea** maana ya kuharisha damu (dk. 10)
- **Wagawe** washiriki katika makundi ya watu 5-7 (dk. 5)
- **Wambie** washiriki wajadili kuhusu dalili za ugonjwa wa kuharisha damu na ruhusu wawasilishe majibu yao kwenye flip chart na toa majumuisho (dk 40)
- **Toa** majumuisho kwa kuoanisha majibu yao na maelezo ya Kitabu cha Mafunzo (dk 10)
- **Elezea** tiba na matumizi bora dawa za kutibu ugonjwa wa Kuharisha damu (dk 10)
- **Elezea** madhara ya dawa ya kutibu ugonjwa wa kuharisha damu (dk 10)
- **Toa** zoezi la kukokotoa dozi ya tiba ya kuhara damu (dk 20)
- **Waelekeze** washiriki mambo muhimu ya kumtaarifa mgonjwa wa kuharisha (dk. 10)
- **Hitimisha** kwa maswali na majibu (dk 10)

## (iii) UGONJWA WA GIARDIA

**Muda: dakika 30**

**Baadhi ya Mbinu za Kufundishia na Kujifunza**

- Mhadhara kwa majadiliano

**Vifaa vya Kufundishia**

- Kitabu cha Mafunzo kwa Watoa Dawa
- Chati pindu (flip chart)
- Gundi ya karatasi
- *Marker pen*
- Ubao na chaki

**Utaratibu wa uwezeshaji:**

- **Tengeneza** mazingira mazuri ya kufundishia (dk. 5)
- **Elezea** maana na dalili muhimu za ugonjwa wa Giardia (dk. 10)
- **Elezea** tiba ya ugonjwa wa Giardia (dk 10)
- **Hitimisha** kwa maswali na majibu (dk 5)

## (iv) KIPINDUPINDU (CHOLERA )

**Muda: Saa 2**

**Baadhi ya Mbinu za Kufundishia na Kujifunza:**

- Mhadhara kwa majadiliano
- Bunga bongo
- Majadiliano katika vikundi ya watu

**Vifaa vya Kufundishia:**

- Kitabu cha Mafunzo kwa Watoa Dawa
- Chati pindu (flip chart)
- Gundi ya karatasi
- *Marker pen*
- Ubao na chaki

**Utaratibu wa uwezeshaji:**

- **Tengeneza** mazingira mazuri ya kufundishia (dk. 5)
- **Soma** malengo ya somo na uyafafanue (dk. 5)
- **Waulize** washiriki wanafahamu nini kuhusu kipindupindu na toa ufafanuzi kwa majibu yaliyotolewa (dk. 10)
- **Wagawe** washiriki katika vikundi vya watu 5-7 (dk 5)
- **Waambie** wajadili jinsi kipindupindu kinavyooenezwa na dalili zake kisha waandike kwenye bango (dk.20)
- **Ruhusu** washiriki vikundi viwasilishe majibu yao ( dk 30)
- toa ufafanuzi kwa majibu yaliyotolewa (dk. 10)
- **Elezea** tiba ya ugonjwa wa Kipindupindu na mambo muhimu ya kukumbuka (dk 10)
- **Waelekeze** washiriki wabunge bongo kuhusu kinga ya ugonjwa wa kipindupindu na toa ufafanuzi (dk 15)
- **Hitimisha** kwa maswali na majibu (dk 10)

## (v) HOMA YA MATUMBO (TYPHOID FEVER)

**Muda:** **Saa 1**

**Baadhi ya Mbinu za Kufundishia na Kujifunza:**

- Mhadhara kwa majadiliano
- Bunga bongo

**Vifaa vya Kufundishia:**

- Kitabu cha Mafunzo kwa Watoa Dawa
- Chati pindu (flip chart)
- Gundi ya karatasi
- *Marker pen*
- Ubao na chaki

**Utaratibu wa uwezeshaji:**

- **Tengeneza** mazingira mazuri ya kufundishia (dk. 5)
- **Eleza** maana ya ugonjwa wa homa ya matumbo (dk 5)
- **Waambie** wabunge bongo kuhusu njia kuu za kueneza ugonjwa wa Homa ya Matumbo (dk 10)
- **Toa** ufafanuzi kuhusu njia kuu za kueneza ugonjwa wa homa ya matumbo.(dk. 10)
- **Elezea** dalili muhimu za ugonjwa wa Homa ya Matumbo (dk. 5)
- **Elezea** tiba ya ugonjwa wa Homa ya Matumbo (dk 5)
- **Waeleze** washiriki wabunge bongo kuhusu kinga ya ugonjwa wa homa ya matumbo (dk 10)
- **Toa** ufafanuzi kuhusu kinga ya ugonjwa wa homa ya matumbo (dk 5)
- **Hitimisha** kwa maswali na majibu (dk 5)

### 3.3.2 MAGONJWA YA MFUMO WA CHAKULA YASIYO YA KUAMBUKIZA

#### (i) MAUMIVU YA TUMBO (*EPIGASTRIC PAIN*)

**Muda:** **Saa 1**

**Baadhi ya Mbinu za Kufundishia na Kujifunza:**

- Mhadhara kwa majadiliano
- Bunga bongo
- Majadiliano katika vikundi

**Vifaa vya Kufundishia:**

- Kitabu cha Mafunzo kwa Watoa Dawa
- Mchoro wa mfumo wa chakula
- Chati pindu (flip chart)
- Gundi ya karatasi
- *Marker pen*
- Ubao na chaki
- Kalamu

**Utaratibu wa uwezeshaji:**

- **Soma** malengo ya somo na uyafafanue (dk. 5)
- **Wambie** washiriki wabunge bongo maana na mambo yanayosababisha maumivu ya tumbo (epigastric pain) (dk 10)
- **Toa** ufafanuzi kuhusu maana na visababishi vya maumivu ya tumbo (dk 10)
- **Eleza** dalili za maumivu ya tumbo (dk 10)
- **Eleza** tiba ya maumivu ya tumbo (dk 10)
- **Waelekeze** washiriki mambo muhimu ya kumtaarifa mgonjwa (dk. 10)
- **Hitimisha** kwa maswali na majibu (dk. 5)

**(ii) KUFUNGA CHOO** *(CONSTIPATION)*

**Muda: Dakika 30**

**Baadhi ya Mbinu za Kufundishia na Kujifunza:**

- Mhadhara kwa majadiliano

**Vifaa vya Kufundishia:**

- Kitabu cha Mafunzo kwa Watoa Dawa
- Chati pindu (flip chart)
- Gundi ya karatasi
- *Marker pen*
- Ubao na chaki
- Kalamu

**Utaratibu wa uwezeshaji:**

- **Tengeneza** mazingira mazuri ya kufundishia (dk. 5)
- **Soma** malengo ya somo na uyafafanue (dk. 5)
- **Eleza** maana na visababishi vya ugonjwa wa Kufunga choo *(constipation)* (dk. 10)
- **Elezea** tiba ya ugonjwa wa Kufunga choo *(constipation)* (dk 5)
- **Hitimisha** kwa kuuliza maswali (dk 5)

**(iii) KUVIMBIWA** *(DYSPEPSIA / INDIGESTION)*

**Muda: Dakika 40**

**Baadhi ya Mbinu za Kufundishia na Kujifunza**

- Mhadhara kwa majadiliano
- Bunga bongo

**Vifaa vya Kufundishia**

- Kitabu cha Mafunzo kwa Watoa Dawa
- Chati pindu (flip chart)
- Gundi ya karatasi
- *Marker pen*
- Ubao na chaki
- Kalamu

**Utaratibu wa uwezeshaji:**

- **Tengeneza** mazingira mazuri ya kufundishia (dk. 5)
- **Wambie** washiriki wabunge bongo maana ya Kuvimbiwa na sababu zake (dk. 5)
- **Elezea** dalili muhimu za Kuvimbiwa (dk. 10)
- **Elezea** tiba ya Kuvimbiwa (dk 10)
- **Waelekeze** washiriki mambo muhimu ya kumtaarifu mgonjwa wa Kuvimbiwa (dk. 5)
- **Hitimisha** maswali na majibu (dk 5)

**(iv) KIUNGULIA (HEARTBURN)**

**Muda: Dakika 50**

**Mbinu ya Kufundisha**

- Mhadhara kwa majadiliano

**Vifaa vya Kufundishia**

- Kitabu cha Mafunzo kwa Watoa Dawa
- Chati pindu (flip chart)
- Gundi ya karatasi
- *Marker pen*
- Ubao na chaki
- Kalamu

**Utaratibu wa uwezeshaji:**

- **Tengeneza** mazingira mazuri ya kufundishia (dk. 5)
- **Waulize** washiriki wanaelewa nini kuhusu kiungulia (dk. 5)
- **Eleza** maana na mambo yanayosababisha Kiungulia (dk. 10)
- **Uliza** washiriki dalili za kiugulia (5)
- **Linganisha** na fafanua majibu ya washiriki (dk. 10)
- **Elezea** tiba ya Kiungulia (dk 10)
- **Hitimisha** kwa maswali na majibu (dk 5)

## (v) VIOTEA KATIKA PURU *(HAEMORRHOIDS / PILES)*

**Muda: Saa 1**

**Baadhi ya Mbinu za Kufundishia na Kujifunza:**

- Mhadhara kwa majadiliano
- Bunga bongo

**Vifaa vya Kufundishia:**

- Kitabu cha Mafunzo kwa Watoa Dawa
- Chati pindu (flip chart)
- Gundi ya karatasi
- *Marker pen*
- Ubao na chaki
- Kalamu

**Utaratibu wa uwezeshaji:**

- **Tengeneza** mazingira mazuri ya kufundishia (dk. 5)
- **Waulize** washiriki wanaelewa nini kuhusu viotea katika puru (dk. 10)
- **Eleza** maana na mambo yanayosababisha viotea katika puru (dk. 15)
- **Uliza** washiriki dalili za viotea katika puru (10)
- **Linganisha** na fafanua majibu ya washiriki (dk. 5)
- **Elezea** tiba ya viotea katika puru (dk 10)
- **Hitimisha** kwa maswali na majibu (dk 5)

## 3.4 SURA YA NNE: MAGONJWA YA MINYOO NA KICHOCHO

**Muda: Saa 7:10**

**Malengo Mahususi ya Sura:**

Ifikapo mwisho wa sura hii washiriki wataweza kueleza:

- Magonjwa ya minyoo yanayojitokeza mara kwa mara, maambikizi na dalili zake
- Tiba sahihi ya magonjwa ya minyoo
- Maudhi na tahadhari kwa dawa za kutibu magonjwa ya Minyoo
- Njia sahihi za kinga ya magonjwa ya minyoo

### 3.4.1 MAGONJWA YA MINYOO

**Muda: Saa 4:30**

**Baadhi ya Mbinu za Kufundishia na Kujifunza:**

- Mhadhara kwa majadiliano
- Bunga bongo
- Majadiliano katika vikundi vidogo vya watu watu 5-6
- Majadiliano katika kikundi kikubwa *(plenary )*

**Vifaa vya Kufundishia:**

- Kitabu cha Mafunzo kwa Watoa Dawa
- Vielelezo vya kinga ya magonjwa ya minyoo
- Chati pindu (flip chart)
- *Marker pens*
- Ubao na chaki
- Picha za minyoo

**Utaratibu wa uwezeshaji 1:**

- **Tengeneza** mazingira mazuri ya kufundishia (dk. 5)
- **Soma** malengo ya somo na uyafafanue (dk. 5)
- **Eleza** kwa kifupi utangulizi wa somo (dk. 5)
- **Eleza** aina za minyoo kama zilivyo kwenye jedwali la minyoo (dk. 10)
- **Gawa** washiriki katika makundi ya watu 5-7 (dk. 5)
- **Vikundi** vijadili jinsi minyoo ya aina mbali mbali inavyoenezwa na dalili zake (dk. 20)
- **Ruhusu** vikundi kuwasilisha majibu yao (dk 45)
- **Toa** ufafanuzi kuhusu njia za uenezwaji na dalili za magonjwa ya minyoo. (dk. 40)

**Utaratibu wa uwezeshaji 2:**

- **Elezea** tiba na maudhi ya Magonjwa ya Minyoo (dk. 30)
- **Toa** maangalizo muhimu kuhusu matumizi bora dawa za kutibu minyoo (dk 30)
- **Gawa** washiriki katika makundi ya watu 5-7 (dk. 5)
- **Vikundi** vijadili ya njia za kuzuia magonjwa ya minyoo (dk 20)
- **Ruhusu** vikundi kuwasilisha majibu yao (30)
- **Linganisha** majibu ya vikundi na maelezo katika kitabu cha mafunzo (dk15)
- **Hitimisha** kwa maswali na majibu (dk. 5)

### 3.4.2 UGONJWA WA KICHOCHO

**Muda: Saa 2:40**

**Baadhi ya Mbinu za Kufundishia na Kujifunza:**

- Mhadhara kwa majadiliano
- Bunga bongo
- Majadiliano katika vikundi
- Ilihali

**Vifaa vya Kufundishia:**

- Kitabu cha Mafunzo kwa Watoa Dawa
- Kielelezo cha maambukizi ya kichocho
- Chati pindu (flip chart)
- Gundi ya Karatasi
- *Marker pens*
- Ubao na chaki
- Ilihali ya kichocho
- Mchoro wa maambukizi ya kichocho

**Utaratibu wa uwezeshaji:**

- **Tengeneza** mazingira mazuri ya kufundishia (dk. 5)
- **Waambie** washiriki wasome ilihali ya kichocho kama ilivyoainishwa katika Kiambatanisho **Na. 5** na pia kwenye kitabu cha mwanafunzi (dk 10)
- **Uliza** maswali kuhusu ilihali ya kichocho (dk 15)
- **Eleza** maana na aina ya ugonjwa wa kichocho (dk. 10)
- **Eleza** maambukizi ya kichocho ya aina mbili za kichocho kwa kutumia mchoro (dk 30)
- **Elezea** dalili za aina mbili za kichocho (dk 15)
- **Elezea** tiba sahihi ya kichocho na maudhi ya dawa hiyo (dk 15)
- **Wape** zoezi la kukokotoa dozi na kozi ya dawa ya kutibu kichocho (dk 20)
- **Fanya** mapitio ya mazoezi uliyowapa ya kukokotoa na toa ufafanuzi (dk 10)
- **Waambie** wabunge bongo kuhusu kinga dhidi ya kichocho (dk 10)
- **Fafanua** na toa majibu sahihi (15)
- **Hitimisha** kwa maswali na majibu (dk 5)

## 3.5 SURA YA TANO: MAGONJWA YA NGOZI

**Muda: Saa 9.45**

**Malengo Mahususi:**

Ifikapo mwisho wa sura hii washiriki wataweza kueleza:

- Aina za magonjwa ya ngozi na dalili zake
- Tiba sahihi za magonjwa ya ngozi
- Namna ya kujikinga na magonjwa ya ngozi

### 3.5.1 MAGONJWA YA NGOZI YANAYOSABABISHWA NA BACTERIA

**Muda: Saa 3**

**Baadhi ya Mbinu za Kufundishia na Kujifunza**

- Mhadhara kwa majadiliano
- Bunga bongo
- Majadiliano katika vikundi

**Vifaa vya Kufundishia**

- Kitabu cha Mafunzo kwa Watoa Dawa
- Chati pindu (flip chart)
- Gundi ya karatasi
- *Marker pens*
- Ubao na chaki
- Picha za magonjwa ya ngozi

**Utaratibu wa uwezeshaji 1: Impetigo: Saa 1**

- **Tengeneza** mazingira mazuri ya kufundishia (dk. 5)
- **Soma** malengo ya somo na uyafafanue (dk. 5)
- **Elezea** utangulizi wa somo (dk. 5)
- **Eleza** dalili za *impetigo* (dk 10)
- **Elezea** tiba ya ugonjwa wa ngozi wa *impetigo* (dk 10)
- **Waulize** washiriki kinga ya impetigo (dk 5)
- Toa majibu sahihi na ufafanuzi (dk 10)
- **Hitimisha** kwa maswali na majibu (dk 10)

**Utaratibu wa uwezeshaji 2: Uvimbe katika mdomo wa tundu la vinyweleo: Dakika 40**

- **Tengeneza** mazingira mazuri ya kufundishia (dk. 5)
- **Elezea** maana ya Uvimbe katika mdomo wa tundu la vinyweleo (dk 5)
- **Eleza** dalili muhimu za Uvimbe katika tundu la vinyweleo (dk. 10)

- **Elezea** tiba ya Uvimbe katika tundu la vinyweleo (dk 10)
- **Hitimisha** kwa maswali na majibu (dk 10)

**Utaratibu wa uwezeshaji 3 : Jipu la ngozi: Dakika 50**

- **Tengeneza** mazingira mazuri ya kufundishia (dk. 5)
- **Eleza** maana ya ugonjwa wa jipu la ngozi kwa kutumia picha au mchoro (dk. 10)
- **Wabunge bongo** dalili za jipu la ngozi (dk. 10)
- **Toa** majibu sahihi na ufafanuzi (dk. 10)
- **Elezea** tiba ya Jipu (dk. 10)
- **Hitimisha** kwa maswali na majibu (dk. 5)

**Utaratibu wa uwezeshaji 4 : Uvimbejoto wa kucha: Dakika 30**

- **Elezea** maana ya ugonjwa wa uvimbejoto wa kucha kwa kutumia picha au mchoro kwa ufafanuzi (dk. 10)
- **Elezea** dalili na tiba ya maambukizi ya kucha (dk.15)
- **Hitimisha** kwa maswali na majibu (dk. 5)

### 3.5.2 MAGONJWA YA NGOZI YANAYOSABABISHWA NA FANGASI

**Muda:** **Saa 4:10**

**Baadhi ya Mbinu za Kufundishia na Kujifunza:**

- Mhadhara kwa majadiliano
- Bunga bongo
- Majadiliano katika vikundi

**Vifaa vya kufundishia:**

- Kitabu cha Mafunzo kwa Watoa Dawa
- Chati pindu (flip chart)
- Gundi ya karatasi
- *Marker pens*
- Ubao na chaki
- Picha ya magonjwa ya ngozi yatokanayo na fangasi

**Utaratibu wa uwezeshaji 1: Mapunye ya ngozi ya mwili: Dakika 45**

- **Tengeneza** mazingira mazuri ya kufundishia (dk. 5)
- **Toa** maelezo kuhusu maana ya mapunye (dk. 5)
- **Uliza** washiriki dalili za mapunye ya ngozi ya mwili (dk 10)
- Toa ufafanuzi na majibu sahihi (dk. 10)
- **Eleza** tiba na ushauri kuhusu mapunye ya mwili (10)
- **Hitimisha** kwa maswali na majibu (dk. 5)

**Utaratibu wa uwezeshaji 2 : Mapunye ya ngozi ya kichwani: Dakika 25**

- **Waambie** washiriki wabunge bongo dalili muhimu za mapunye ya ngozi ya kichwani (dk. 10)
- **Elezea** pale waliposhindwa kutaja dalili muhimu za mapunye ya ngozi ya kichwani (dk. 5)
- **Elezea** tiba ya mapunye ya ngozi ya kichwani (dk 10)

**Utaratibu wa uwezeshaji 3 : Mba : Dakika 30**

- **Waambie** washiriki wabunge bongo kuhusu dalili za mba (dk 10)
- **Elezea** pale waliposhindwa kutaja dalili muhimu za mba (dk. 10)
- **Elezea** tiba ya mba (dk 10)

**Utaratibu wa uwezeshaji 4 - Fangasi za miguu: Dakika 30**

- **Waambie** washiriki wabunge bongo kuhusu maana na dalili za fangasi wa miguu (dk 10)
- **Elezea** pale waliposhindwa kutaja dalili muhimu za Fangasi za miguu (dk. 10)
- **Elezea** tiba ya Fangasi za miguu (dk 10)

**Utaratibu wa uwezeshaji 5 : Kandida (Kuvu)    Saa  2**

- **Tengeneza** mazingira mazuri ya kufundishia (dk. 5)
- **Elezea** maana ya kandida na makundi yake (dk 10)
- **Wagawe** washiriki katika makundi ya watu 5-7 (dk. 5)
- **Wambie** kila kundi litajadili dalili za aina mojawapo  ya ugonjwa wa kandida (dk. 15)
- **Ruhusu** kila kundi kuwasilisha majibu yake (dk 40)
- **Elezea** pale waliposhindwa kutaja dalili muhimu za Kandida kwa kuzingatia Kitabu cha Mwanafunzi (dk. 10)
- **Elezea** tiba ya Kandida (dk 30)
- **Hitimisha** kwa maswali na majibu (dk 5)

### 3.5.3 MAGONJWA YA NGOZI YANAYOSABABISHWA NA VIRUSI (MKANDA WA JESHI - *Herpes Zooster*)

**Muda:** **Dakika 35**

**Baadhi ya Mbinu za Kufundishia na Kujifunza:**

- Mhadhara kwa majadiliano
- Bunga bongo
- Majadiliano katika vikundi

**Vifaa vya Kufundishia:**

- Kitabu cha Mafunzo kwa Watoa Dawa
- Vielelezo – Picha ya mtu mwenye Mkanda wa Jeshi
- Chati pindu (flip chart)
- Gundi ya Karatasi
- *Marker pens*
- Ubao na chaki

**Utaratibu wa uwezeshaji:**

- **Tengeneza** mazingira mazuri ya kufundishia (dk. 5)
- **Wambie** washiriki wabunge bongo maana na dalili ya Mkanda wa Jeshi (dk. 10)
- Toa ufafanuzi na majibu sahihi kwa kuzingatia Kitabu cha Mwanafunzi (dk.10)
- **Elezea** tiba ya Mkanda wa Jeshi (dk. 5)
- **Hitimisha** kwa maswali na majibu (dk. 5)

### 3.5.4 MAGONJWA YA NGOZI YANAYOSABABISHWA NA *PARASITES* (UPELE - *SCABIES*)

**Muda: Saa 1**

**Baadhi ya Mbinu za Kufundishia na Kujifunza**

- Mhadhara kwa majadiliano
- Bunga bongo

**Vifaa vya Kufundishia**

- Kitabu cha Mafunzo kwa Watoa Dawa
- Chati pindu (flip chart)
- Gundi ya karatasi
- *Marker pens*
- Ubao na chaki
- Picha

**Utaratibu wa uwezeshaji :**

- **Waambie** wabunge bongo maana ya upele na dalili zake (dk 10)
- **Toa** ufafanuzi wa maana na dalili kulingana na Kitabu Cha Mwanafunzi (dk. 5)
- **Elezea** tiba ya Upele (dk. 15)
- **Waambie** wabunge bongo kuhusu kinga ya upele (dk 15)
- **Toa** ufafanuzi kwa kusisitiza mambo muhimu katika kinga ya upele (dk 10)
- **Hitimisha** kwa maswali na majibu (dk 5)

### 3.5.5 MAGONJWA YA NGOZI YANAYOSABABISHWA NA MZIO (*ALLERGY*)

**Muda: Saa 1**

**Baadhi ya Mbinu za Kufundishia na Kujifunza**

- Mhadhara kwa majadiliano
- Bunga bongo

**Vifaa vya Kufundishia**

- Kitabu cha Mafunzo kwa Watoa Dawa
- Vielelezo
- Chati pindu (flip chart)
- Gundi ya karatasi
- *Marker pens*
- Ubao na chaki
- Kalamu

**Utaratibu wa uwezeshaji:**

- **Tengeneza** mazingira mazuri ya kufundishia (dk. 5)
- **Elezea** maana ya mzio (dk. 10)
- **Waambie** washiriki wabunge bongo kuhusu visababishi vya mzio wa ngozi (dk 10)
- **Toa** ufafanuzi kuhusu visababishi vya mzio (dk 10)
- **Elezea** tiba ya magonjwa ya ngozi yanayosababishwa na mzio (dk. 10)
- **Elezea** maudhi ya dawa ya kutibu magonjwa ya ngozi yanayosababishwa na mzio (dk. 10)
- **Hitimisha** kwa maswali na majibu (dk 5)

## 3.6 SURA YA SITA: MAGONJWA YA MASIKIO NA MACHO

**Muda: saa 2**

**Malengo Mahususi**

Ifikapo mwisho wa sura hii washiriki kueleza:

- Dalili za magonjwa ya masikio na macho
- Tiba ya magonjwa ya masikio na macho
- Kinga ya magonjwa ya masikio na macho

### 3.6.1 UGONJWA WA SIKIO *(OTITIS MEDIA)*

**Muda: Saa 1**

**Baadhi ya Mbinu za Kufundishia na Kujifunza**

- Mhadhara kwa majadiliano
- Majadiliano katika vikundi

**Vifaa vya Kufundishia**

- Kitabu cha Mafunzo kwa Watoa Dawa
- Mchoro au picha ya sikio au *model*
- Chati pindu (flip chart)
- Gundi ya karatasi
- *Marker pens*
- Ubao na chaki
- Kalamu

**Utaratibu wa uwezeshaji**

- **Tengeneza** mazingira mazuri ya kufundishia (dk. 5)
- **Soma** malengo ya somo na uyafafanue (dk. 5)
- **Elezea** maana ya uvimbe wa sikio la kati (dk. 5)
- **Wagawe** washiriki katika makundi ya watu 5-7 (dk 5)
- **Waambie** wajadili dalili za Uvimbe wa sikio la kati na wawasilishe kwenye kundi kubwa (dk 15)
- **Toa** ufafanuzi na majumuisho (dk 10)
- **Elezea** tiba ya Uvimbe wa sikio la kati (dk 10)
- **Hitimisha** kwa maswali na majibu (dk 5)

### 3.6.2 UGONJWA WA MACHO (Uvimbejoto wa Konjaktiva) *(Conjunctivitis*)

**Muda: Saa 1**

**Baadhi ya Mbinu za Kufundishia na Kujifunza**

- Mhadhara kwa majadiliano
- Majadiliano katika vikundi
- Majadiliano katika kikundi kikubwa (plenary )

**Vifaa vya Kufundishia**

- Kitabu cha Mafunzo kwa Watoa Dawa
- Picha au Mchoro wa jicho au *model*
- Chati pindu (flip chart)
- Gundi ya karatasi
- *Marker pens*
- Ubao na chaki
- Kalamu

**Utaratibu wa uwezeshaji:**

- **Tengeneza** mazingira mazuri ya kufundishia (dk. 5)
- **Elezea** maana ya Uvimbejoto wa konjaktiva *(conjunctivitis)* (dk. 5)
- **Wagawe** washiriki katika makundi ya watu 5-7 (dk 5)
- **Waambie** wajadili dalili za Uvimbejoto wa konjaktiva *(conjunctivitis)*na wawasilishe kwenye kundi kubwa (dk 10)
- **Toa** ufafanuzi na majumuisho (dk 10)
- **Elezea** tiba ya Uvimbejoto wa konjaktiva *(conjunctivitis)* (dk 10)
- **Eleza** tahadhari na kinga ya magonjwa ya macho (10)
- **Hitimisha** kwa maswali na majibu (dk 5)

## 3.7 SURA YA SABA: SHINIKIZO LA JUU LA DAMU *(HYPERTENSION)*

**Muda:** **Saa 2**

**Malengo mahsusi**
Ifikapo mwisho wa sura hii washiriki wataweza kuelezea:

- Kuelezea maana ya shinikizo la juu la damu na sababu zinazochangia kuwepo kwake
- Dalili za shinikizo la juu la damu
- Tiba ya shinikizo la juu la damu

**Baadhi ya Mbinu za Kufundishia na Kujifunza**

- Mhadhara wa majadiliano
- Bunga bongo
- Majadiliano katika kikundi

**Vifaa vya Kufundishia**

- Kitabu cha Mafunzo kwa Watoa Dawa
- Chati pindu (flip chart)
- Gundi karatasi
- *Marker pen*
- Ubao na chaki

**Utaratibu wa uwezeshaji:**

- **Tengeneza** mazingira mazuri ya kufundishia (dk 5)
- **Onesha** na fafanua malengo ya sura yaliyoandikwa kwenye Chati pindu (flip chart) (dk.5)
- **Waambie** washiriki wabunge bongo maana na sababu za shinikizo la juu la damu (dk.10)
- **Linganisha** mambo yaliyotajwa na maelezo ya maana na sababu za shinikizo la juu la damu kama yalivyo kwenye Kitabu cha Mafunzo (dk. 10)
- **Gawa** washiriki katika makundi ya watu 5-7 (dk 5)
- **Waambie wajadili** kuhusu dalili muhimu za shinikizo la juu la damu (dk. 10)
- **Ruhusu** kila kikundi wawasilishe mambo waliyojadiliana (dk. 40)
- **Linganisha** mambo waliowasilisha na maelezo yaliyomo kwenye kitabu cha mafunzo kwa kutoa mifano (dk. 10)
- **Elezea** tiba ya shinikizo la juu la damu (dk. 10)
- **Elezea** mambo muhimu ya kukumbuka kuhusiana na shinikizo la juu la damu (dk. 10)
- **Hitimisha** kwa maswali na majibu (dk. 5)

## 3.8 SURA YA NANE: MAUMIVU NA UVIMBEJOTO (PAIN AND INFLAMATION)

**Muda:** **Saa 2**

**Malengo ya Sura:**

Ifikapo mwisho wa sura hii washiriki wataweza:

- Kuelezea maumivu na uvimbejoto na sababu zinazochangia kuwepo kwake.
- Kuelezea dalili za maumivu na uvimbejoto
- Kuelezea tiba ya maumivu na uvimbejoto

**Baadhi ya Mbinu za Kufundishia na Kujifunza**

- Mhadhara wa majadiliano
- Majadiliano katika vikundi

**Vifaa vya Kufundishia**

- Kitabu cha Mafunzo kwa Watoa Dawa
- Chati pindu (flip chart)
- Gundi ya karatasi
- *Marker pen*
- Ubao na chaki

**Utaratibu wa uwezeshaji :**

- **Tengeneza** mazingira mazuri ya kufundishia *(Climate Setting)* (dk 5)
- **Onesha** na fafanua malengo ya sura yaliyoandikwa kwenye Chati pindu (flip chart) (dk.5)
- **Eleza** dalili za maumivu na uvimbejoto (dk. 10)
- **Eleza** tiba ya maumivu na uvimbejoto (dk. 30)
- **Toa** zoezi la kutoa dawa za maumivu na uvimbejoto kwa watu wa rika tofauti (dk 20)
- **Eleza** tahadhari kuhusu tiba ya maumivu na uvimbejoto (dk.20)
- **Eleza** maudhi ya dawa za tiba ya maumivu na uvimbe joto (dk. 10)
- **Eleza** maumivu wakati wa hedhi *(dysmenorrhoea)* na tiba yake(dk. 10)
- **Hitimisho** (dk. 10)

## 3.9 SURA YA TISA: MSHITUKO WA ANAFILAKSIA (ANAPHYLACTIC SHOCK)

**Muda: Dakika 45**

**Malengo Mahususi ya Sura:**

Ifikapo mwisho wa sura hii washiriki wataweza kueleza:

- Maana na chanzo cha mshituko wa anafilaksia
- Dalili za mshituko wa anafilaksia
- Hatua za kuchukua kwa mgonjwa mwenye mshituko wa anafilaksia

**Baadhi ya Mbinu za Kufundishia na Kujifunza**

- Mhadhara kwa majadiliano
- Bunga bongo
- Majadiliano katika vikundi vidogo

**Vifaa vya Kufundishia**

- Kitabu cha Mafunzo kwa Watoa Dawa
- Vielelezo
- Gundi ya karatasi
- *Marker pens*
- Ubao na chaki
- Kalamu

**Utaratibu wa uwezeshaji :**

- **Tengeneza** mazingira mazuri ya kufundishia (dk 5)
- **Soma** malengo ya somo na uyafafanue (dk. 5)
- **Eleza** maana ya mshituko wa anafilaksia (dk 5)
- **Uliza** washiriki dalili za mshituko wa anafilaksia *(anaphylactic shock)* (dk 5)
- **Toa** ufafanuzi kuhusu dalili za mshituko wa anafilaksia (dk 10)
- **Elezea** tiba ya mshituko wa anafilaksia (dk 10)
- **Hitimisha** kwa maswali na majibu (dk 5)

## Kuhitimisha moduli

**Utaratibu wa uwezeshaji: dk 35**

- **Uliza** eneo ambalo linahitaji ufafanuzi katika sura zote (dk 5)
- **Fanya** majumuisho ya mambo ya msingi kwa kila sura (dk 10)
- **Fanya** tathmini moduli kwa kuwataka washiriki wajaze dodoso la tathmini (dk 20)

# Moduli ya Nne

## 4.0 MODULI YA NNE : AFYA YA UZAZI

**Muda wa Moduli: saa 17.00**

**Utangulizi wa Moduli**

**Utaratibu wa uwezeshaji : Dakika 25**

- **Tengeneza** mazingira mazuri ya kufundishia (dk. 5)
- **Elezea** utangulizi wa moduli (dk. 5)
- **Elezea** lengo la moduli (dk. 5)
- **Taja** sura zilizoko katika moduli (dk. 5)
- **Wafahamishe** jinsi watakavyotathminiwa (dk. 5)

## 4.1 SURA YA KWANZA : UZAZI WA MPANGO

**Muda: Saa 5**

**Malengo Mahsusi:**

Ifikapo mwisho wa sura hii washiriki wataweza kueleza:

- Mfumo wa uzazi
- Njia teule za uzazi wa mpango zilivyoruhusiwa kwenye DLDM
- Mambo muhimu ya kuhakiki kabla ya kumuanzishia mteja vidonge vya kumeza vyenye vichecheo viwili
- Namna ya kutumia vidonge vya uzazi wa mpango
- Njia ya dharura ya vidonge vya uzazi wa mpango
- Njia za uzazi wa mpango wa kondom ya kiume /kike
- Njia ya asili ya uzazi wa mpango ya unyonyeshaji baada ya kujifungua

**Baadhi ya Mbinu za Kufundishia na Kujifunza**

- Mhadhara kwa majadiliano
- Bunga bongo
- Majadiliano katika kikundi
- Igizo

**Vifaa vya Kufundishia**

- Kitabu cha Mafunzo kwa Watoa Dawa
- Chati pindu (flip chart)
- Gundi ya karatasi
- *Marker pen*
- Ubao na chaki

- Kondumu za kike na kiume
- Sampuli za vidonge vya uzazi wa mpango
- *Models* na picha za viungo vya kiume na kike

**Utaratibu wa uwezeshaji 1: Dakika 30**

- **Tengeneza** mazingira mazuri ya kufundishia (dk 5)
- **Onesha** na fafanua malengo ya sura yaliyoandikwa kwenye Chati pindu (flip chart) (dk.5)
- **Toa** maelezo kuhusu mfumo wa uzazi (dk 20)

**Utaratibu wa uwezeshaji 2 : Saa 3**

- **Waambie** washiriki wabunge bongo njia za uzazi wa mpango zinazotumika Tanzania (dk 15)
- **Toa** ufafanuzi kwa kuainisha njia za uzazi wa mpango zinazoruhusiwa na zisizoruhusiwa kwenye DLDM (dk. 10)
- **Elezea** njia ya uzazi wa mpango za vidonge vyenye vichocheo viwili (dk. 30)
- **Elezea** mambo ya kuthibitisha kabla ya kumwanzishia mteja vidonge vya uzazi wa mpango (dk 15)
- **Eleza** namna ya kutumia vidonge vya uzazi wa mpango (dk 20)
- **Gawa** washiriki katika makundi ya watu 5- 10 (dk 5)
- **Waambie** kila kikundi kiteue washiriki wawili mmoja achukue nafasi ya Mtoa Dawa na mwingine nafasi ya mteja (dk 5)
- **Waambie** wafanye zoezi kwa vitendo katika makundi yao la jinsi watakavyomwanzishia mteja vidonge vya uzazi wa mpango (dk. 25)
- **Teua** kundi moja lifanye zoezi hilo kwa darasa zima (dk 20)
- **Toa** majumuisho ya zoezi ukiainisha njia sahihi ya kumwanzishia mteja vidonge vya uzazi wa mpango (dk 20)
- **Eleza** njia ya dharura ya vidonge vya uzazi wa mpango (dk 15)

**Utaratibu wa uwezeshaji 3: Saa 1.30**

- **Tengeneza** mazingira mazuri ya kufundishia (dk 5)
- **Toa** maelezo ya jinsi ya kutumia kutumia kondomu ya kike (dk 15)
- **Onesha** njia sahihi za matumizi ya kondomu ya kike (15)
- **Toa** maelezo ya jinsi ya kutumia kondomu ya kiume (dk 15)
- **Onesha** njia sahihi ya matumizi ya kondomu ya kiume (dk 15)

- **Elezea** njia ya asili ya uzazi wa mpango ya unyonyeshaji baada ya kujifungua (dk 15)
- **Hitimisha** somo kwa maswali na majibu (dk 10)

## 4.2 SURA LA PILI: MAGONJWA YAENEZWAYO KWA NJIA YA KUJAMIIANA

**Muda:** **Saa 4**

**Malengo Mahsusi**

Ifikapo mwisho wa sura hii washiriki wataweza kueleza:

- Dalili za magonjwa yatokanayo na kujamiiana
- Ngazi mbili za tiba ya magonjwa yatokanayo na kujamiiana
- Mambo muhimu ya kuzingatia wakati wa kutoa ushauri kuhusu magonjwa ya kujamiiana

**Baadhi ya Mbinu za Kufundishia na Kujifunza**

- Mhadhara wa majadiliano
- Bunga bongo
- Majadiliano katika vikundi
- Igizo

**Vifaa vya Kufundishia**

- Kitabu cha Mafunzo kwa Watoa Dawa
- Vielelezo
- Maelezo ya igizo
- Picha ya video
- Mabango ya magonjwa ya kujamiiana
- Chati pindu (flip chart)
- Gundi ya karatasi
- *Marker pen*
- Ubao na chaki

**Utaratibu wa uwezeshaji 1:** **Dakika 30**

- **Tengeneza** mazingira mazuri ya kufundishia (dk 5)
- **Onesha** na fafanua malengo ya sura yaliyoandikwa kwenye Chati pindu (flip chart) (dk.5)
- **Toa** utangulizi wa sura ukisisitiza umuhimu wa kutibu magonjwa haya haraka na kikamilifu (dk 10)
- **Waambie** washiriki wabunge bongo kuhusu magonjwa na dalili za magonjwa ya kujamiiana (dk 10)

**Utaratibu wa uwezeshaji 2:** **Saa 3:30**

- **Elezea** mkusanyiko wa dalili za magonjwa yaenezwayo kwa kujamiiana (dk 45)
- **Elezea** tiba ya magonjwa ya kujamiiana kwa kuzingatia mkusanyiko wa dalili (dk 45)

- Waambie wabunge bongo kuhusu tahadhari na kinga ya magonjwa ya kujamiiana (dk 10)
- **Toa** ufafanuzi wa tahadhari na kinga ya magonjwa ya kujamiiana (dk 15)
- **Teua** washiriki watatu mmoja Mtoa Dawa, mwingine mgonjwa na mwenza wa mgonjwa (dk 5)
- **Wape** maelezo juu ya zoezi la kumshawishi mwenza kupata tiba ya magonjwa ya kujamiiana. Maelezo haya yatolewe bila ya washiriki wengine kusikia (dk 10)
- **Ruhusu** waoneshe igizo la kumshawishi mwenza kupata tiba ya magonjwa ya kujamiiana kwa darasa zima (dk 30)
- **Ruhusu** majadiliano katika kundi kubwa (dk 10)
- **Toa** majumuisho ya hatua za kufuata katika kumsaidia mgonjwa jinsi ya kumshawishi mwenza kutibiwa magonjwa ya kujamiiana (dk 30)
- **Hitimisha** kwa maswali na majibu (dk 10)

## 4.3 SURA YA TATU: VIRUSI VYA UKIMWI NA UKIMWI

**Muda:** **Saa 7:35**

**Malengo ya Sura:**

Ifikapo mwisho wa sura hii washiriki wataweza kuelezea:

- Maana ya Virusi vya UKIMWI (VVU) na UKIMWI, jinsi ya kuambukizwa, dalili zake na kinga
- Faida za kupima VVU na ushauri nasaha
- Tiba ya magonjwa nyemelezi iliyoidhinishwa kwenye DLDM
- Unyanyapaa kwa wagonjwa wa UKIMWI
- Wajibu wa Mtoa Dawa katika kutokomeza unyanyapaa

**Baadhi ya Mbinu za Kufundishia na Kujifunza**

- Mhadhara wa Majadiliano
- Bunga bongo
- Majadiliano katika vikundi
- Igizo

**Vifaa vya Kufundishia**

- Kitabu cha Mafunzo kwa Watoa Dawa
- Chati pindu (flip chart)
- Gundi ya karatasi
- *Marker pen*
- Ubao na chaki
- Picha za video
- Kitabu cha takwimu za UKIMWI

**Utaratibu wa uwezeshaji 1:** **Saa 1**

- **Tengeneza** mazingira mazuri ya kufundishia (dk 5)
- **Onesha** na fafanua malengo ya sura yaliyoandikwa kwenye Chati pindu (flip chart) (dk.5)
- **Onesha** mkanda wa video wa UKIMWI (dk 35)
- **Toa** utangulizi wa sura juu ya ukubwa wa tatizo la UKIMWI nchini (dk 15)

**Utaratibu wa uwezeshaji 2:** **Saa 2**

- **Wagawe** washiriki katika makundi (dk. 5)
- **Waambie** kila kundi lijadili maambukizi, dalili na kinga dhidi ya UKIMWI(dk. 5)
- **Ruhusu** majadiliano (dk. 30)
- **Ruhusu** kila kundi liwasilishe kwa dakika 5 (dk. 35)
- **Linganisha** mambo waliowasilisha ukionisha maelezo kuhusu maambukizi dalili, na kinga dhidi ya UKIMWI kama ilivyoainishwa kwenye Kitabu cha Mafunzo (dk.45)

**Utaratibu wa uwezeshaji 3: Saa 1**

- **Wambie** washiriki wabunge bongo kuhusu faida ya kufahamu kama una VVU ukiandika majibu yao kwenye Chati pindu (flip chart) (dk. 20)
- **Linganisha** mambo yaliyotajwa na maelezo ya faida kama yalivyo kwenye Kitabu Cha Mafunzo (dk. 30)
- **Eleza** faida ya ushauri nasaha kuhusu VVU (dk. 10)

**Utaratibu wa uwezeshaji 4: Saa 3**

- **Eleza** tiba ya magonjwa nyemelezi kama ilivyo kwenye Kitabu Cha Mafunzo (dk. 20)
- **Waambie** washiriki wabunge bongo kuhusu majukumu ya Mtoa Dawa katika kupiga vita UKIMWI (dk. 20)
- **Linganisha** majibu waliowasilisha ukioanisha na maelezo yaliyoko kwenye Kitabu cha Mafunzo (dk.15)
- **Wagawe** washiriki katika makundi (dk. 5)
- **Waambie** kila kundi lijadili wanaelewa nini kuhusu unyanyapaa na madhara yake pamoja na majukumu ya Mtoa Dawa katika kutokomeza unyanyapaa (dk. 5)
- **Ruhusu** majadiliano (dk. 30)
- **Ruhusu** kila kundi liwasilishe kwa dakika 5 (dk. 40)
- **Linganisha** majibu waliowasilisha ukioanisha na maelezo yaliyoko kwenye Kitabu cha Mafunzo (dk.35)
- **Hitimisha** somo kwa maswali na majibu (dk 10)

**Kuhitimisha moduli**

**Utaratibu wa uwezeshaji: dk 35**

- **Uliza** eneo ambalo linahitaji ufafanuzi katika sura zote (dk 5)
- **Fanya** majumuisho ya mambo ya msingi kwa kila sura (dk 10)
- **Fanya** tathmini ya moduli kwa kuwataka washiriki wajaze dodoso la tathmini (dk 20)

# Moduli ya Tano

## 5.0 MODULI YA TANO: STADI ZA MAWASILIANO

**Muda wa Moduli:** **saa 9:10**

**Utangulizi wa Moduli**

**Utaratibu wa uwezeshaji (*Task*):** **Dakika 25**

- **Tengeneza** mazingira mazuri ya kufundishia (dk. 5)
- **Elezea** utangulizi wa moduli (dk. 5)
- **Elezea** lengo la moduli (dk. 5)
- **Taja** sura zilizoko katika moduli (dk. 5)
- **Wafahamishe** jinsi watakavyotathminiwa (dk. 5)

## 5.1 SURA YA KWANZA: KUJENGA NA KUDUMISHA UHUSIANO BORA KATIKA DLDM

**Muda:** **Saa 2:30**

**Malengo Mahsusi**

Ifikapo mwisho wa sura hii washiriki wataweza kueleza:

- Faida za kujenga na kudumisha uhusiano bora kwenye DLDM
- Stadi na mbinu za mawasiliano katika kuboresha huduma kwenye DLDM

**Baadhi ya Mbinu za Kufundishia na Kujifunza**

- Mhadhara wa majadiliano
- Bunga bongo
- Majadiliano katika vikundi
- Igizo

**Vifaa vya Kufundishia**

- Kitabu cha Mafunzo kwa Watoa Dawa
- Vielelezo
- Maelezo ya igizo
- Chati pindu (flip chart)
- Gundi ya karatasi
- *Marker pen*
- Ubao na chaki
- Picha za video

**Utaratibu wa uwezeshaji 1:** **Dakika 20**

- **Tengeneza** mazingira mazuri ya kufundishia (dk 5)
- **Onesha** na fafanua malengo ya sura yaliyoandikwa kwenye Chati pindu (flip chart) (dk.5)
- **Toa** utangulizi wa sura (dk 10)

**Utaratibu wa uwezeshaji 2: Saa 2:10**

- **Teua** washiriki 3 na wape maelezo ya maandishi ya igizo *(script)* kuhusu stadi za mawasiliano yaliyo kwenye kiambatanisho **Na. 10** na kitabu cha mwanafunzi angalau siku moja kabla ya somo (dk 5)
- **Ruhusu** washiriki walioteuliwa kufanya igizo la stadi za mawasiliano kwa darasa zima (dk 25)
- **Ruhusu** majadiliano kuhusu stadi za mawasiliano (dk 20)
- **Fafanua** stadi na mbinu za mawasiliano katika uendeshaji wa DLDM kwa kuzingatia kitabu cha mafunzo (dk 30)
- **Waambie** washiriki wabunge bongo kuhusu faida za kuwa na uhusiano bora kwenye DLDM (dk. 10)
- **Linganisha** majibu waliowasilisha ukioanisha faida za kuwa na uhusiano bora kwenye DLDM na maelezo yaliyoko kwenye Kitabu cha Mafunzo (dk 30)
- **Hitimisha** kwa maswali na majibu (dk. 10)

## 5.2 SURA YA PILI: ELIMU YA AFYA KWA MTEJA

**Muda: Saa 3:35**

Ifikapo mwisho wa sura hili washiriki wataweza kueleza:

- Umuhimu wa kutoa elimu ya afya katika DLDM
- Hatua za kutoa elimu ya afya
- Namna ya kuboresha utoaji elimu ya afya katika DLDM

**Baadhi ya Mbinu za Kufundishia na Kujifunza**

- Mhadhara wa majadiliano
- Bunga bongo
- Majadiliano katika vikundi

**Vifaa vya Kufundishia**

- Kitabu cha Mafunzo kwa Watoa Dawa
- Chati pindu (flip chart)
- Gundi ya karatasi
- "Marker pen"
- Ubao na chaki

**Utaratibu wa uwezeshaji 1: Dakika 20**

- **Tengeneza** mazingira mazuri ya kufundishia (dk 5)
- **Onesha** na fafanua malengo ya sura yaliyoandikwa kwenye Chati pindu (flip chart) (dk.5)
- **Fafanua** malengo ya sura (dk. 5)
- **Toa** utangulizi wa sura (dk 5)

**Utaratibu wa uwezeshaji 2: Saa 1:15**

- **Wagawe** washiriki katika makundi ya watu 5-7(dk. 5)
- **Waambie** kila kundi lijadili umuhimu wa kutoa elimu ya afya katika DLDM (dk. 20)
- **Ruhusu** kila kundi liwasilishe (dk. 40)
- **Linganisha** majibu waliowasilisha ukioanisha na maelezo yaliyoko kwenye Kitabu cha Mafunzo (dk.10)

**Utaratibu wa uwezeshaji 3: Saa 2**

- **Elezea** mambo ya kuzingatia katika kutoa elimu ya afya (dk 10)
- **Wagawe** washiriki katika makundi (dk. 5)
- **Teua** washiriki wawili na wape maelezo ya maandishi ya zoezi kwa vitendo kuhusu elimu ya afya kwa mteja katika DLDM kama iliyoanishwa katika kiambatanisho **Na. 8** na kwenye kitabu cha mwanafunzi (dk 5)

- **Ruhusu** washiriki walioteuliwa kufanya igizo la elimu ya afya kwa mteja katika DLDM kwa darasa zima (dk 25)
- **Ruhusu** majadiliano kuhusu elimu ya afya kwa mteja katika DLDM(dk 20)
- **Fafanua** elimu ya afya kwa mteja katika DLDM kwa kuzingatia kitabu cha mafunzo (dk 15)
- **Waambie** washiriki wabunge bongo kuhusu mambo yanayozorotesha utoaji wa elimu ya afya kwenye DLDM (dk. 10)
- **Linganisha** majibu waliowasilisha ukioanisha na maelezo yaliyoko kwenye Kitabu cha Mafunzo (dk.20)
- **Hitimisha** kwa maswali na majibu (dk. 10)

## 5.3 SURA YA TATU: USHAURI NASAHA KATIKA DLDM

**Muda: Saa 2:30**

**Malengo Mahsusi**

Ifikapo mwisho wa sura hii washiriki wataweza kueleza:

- Mambo muhimu yanayofanana na kutofautiana kati ya elimu ya afya na ushauri nasaha
- Matukio yanayostahili ushauri nasaha katika DLDM
- Hatua za kufuata wakati wa kutoa ushauri nasaha kwa mteja

**Baadhi ya Mbinu za Kufundishia na Kujifunza**

- Mhadhara kwa majadiliano
- Mazoezi kwa vitendo
- Bunga bongo
- Majadiliano katika vikundi

**Vifaa vya Kufundishia**

- Kitabu cha Mafunzo kwa Watoa Dawa
- Vielelezo
- Maelezo ya zoezi kwa vitendo
- Chati pindu (flip chart)
- Gundi ya karatasi
- *Marker pen*
- Ubao na chaki

**Utaratibu wa uwezeshaji 1: Saa 1**

- **Tengeneza** mazingira mazuri ya kufundishia (dk 5)
- **Onesha** na fafanua malengo ya sura yaliyoandikwa kwenye Chati pindu (flip chart) (dk.5)
- **Toa** utangulizi wa sura (dk 5)
- **Eleza** mambo yanayofanana na kutofautiana kati ya elimu ya afya na ushauri nasaha (dk. 15)
- **Eleza** matokeo ya ushauri nasaha (dk. 15)
- **Waambie** washiriki wabunge bongo kuhusu matukio na matatizo yanayotakiwa kutolewa ushauri nasaha (dk 10)
- **Fanya** majumuisho ya matukio na matatizo yanayotakiwa kutolewa ushauri nasaha kwa kuoanisha yaliyomo kwenye Kitabu cha Mtoa Dawa (dk 5)

**Utaratibu wa uwezeshaji 2: Saa 1.30**

- **Teua** washiriki wawili (mmoja kama mtoa dawa, mwingine mteja) na wape maelezo ya maandishi *(script)* ya igizo dhima jinsi ya kutoa ushauri nasaha kwa usahihi agalau siku moja kabla ya somo- angalia kiambatanisho **Na. 9** na kwenye kitabu cha mwanafunzi (dk 5)

- **Ruhusu** washiriki walioteuliwa kuigiza jinsi ya kutoa ushauri nasaha kwa usahihi kwa darasa zima (dk 15)
- **Ruhusu** majadiliano kuhusu hatua za kufuata katika kutoa ushauri nasaha (dk 20)
- **Fafanua** hatua za kufuata katika kutoa ushauri nasaha kwa kuzingatia kitabu cha mafunzo (dk 25)
- **Eleza** mambo muhimu ya kufaya unapompa mteja rufaa (dk.15)
- **Hitimisha** kwa maswali na majibu (dk. 10)

**Kuhitimisha moduli**

**Utaratibu wa uwezeshaji: Dakika 35**

- **Uliza** eneo ambalo linahitaji ufafanuzi katika sura zote (dk 5)
- **Fanya** majumuisho ya mambo ya msingi kwa kila sura (dk 10)
- **Fanya** tathmini ya moduli kwa kuwataka washiriki wajaze dodoso la tathmini (dk 20)

# Hitimisho la Mafunzo

## TATHMINI YA MAFUNZO

Tathmini ya Mafunzo ya Watoa Dawa katika DLDM itafanyika baada ya mwanafunzi kusoma moduli zote kwa lengo la kubaini kama malengo ya mafunzo yamefikiwa. Aidha, inalenga kupima uelewa wa washiriki baada ya mafunzo. Matokeo ya tathmini yatasadia kuboresha mafunzo haya siku za usoni.

**Muda** **Saa 8.00**

**Utaratibu wa kufanya tathmini** **saa 8.00**

- **Watake** washiriki watathmini uendeshaji wa mafunzo kwa kujaza fomu maalum
- **Watake** wawezeshaji kutathmini uendeshaji wa mafunzo kwa kujaza fomu maalum (Saa 1)
- **Toa** mrejesho kwa washiriki kuhusu tathmini ya mafunzo (Saa 1)
- **Toa** mtihani wa mwisho wa mafunzo (Saa 6)

# Viambatanisho

## Kiambatanisho 1

## ILIHALI (MODULI 1; SURA 1)

## MAKOSA NA ADHABU ZA UVUNJAJI WA KANUNI ZA DLDM

Mwendapole ni mkazi wa kijiji cha Nakapanya, alipata shauku kubwa ya kuanzisha Duka la dawa baada ya kumtembelea rafiki yake Ngonyani ambaye alikuwa na duka la dawa mjini Mbinga. Mwendapole alituma maombi ya kuanzisha Duka la dawa kupitia ngazi zote na hatimaye, baada ya yeye na mtoa dawa kuhudhuria mafunzo, alifanikiwa kuanzisha Duka hilo.

Mwendapole alitarajia kupata faida na hatimaye kujenga nyumba ya kisasa. Ili aweze kupata faida ya kutosha alitafuta dawa kutoka vyanzo mbalimbali ikiwa ni pamoja na kununua dawa kutoka kwa wafanyabiashara ya mkononi na dawa zilizochukuliwa kutoka hospitali za misheni na hospitali za serikali. Ili kuhakikisha anauza sana alimwamuru mtoa dawa auze dawa bila kujali kama mgonjwa ana cheti cha mganga au dawa zimeisha muda wa matumizi. Ili kupunguza gharama za uendeshaji alimfukuza mtoa dawa na nafasi yake kuchukuliwa na mkewe ambaye alikuwa mama wa nyumbani. Mke wake Mwendapole alikuwa hajui kuandika.

Baada ya miezi sita wakaguzi kutoka wilayani walifika na baada ya ukaguzi waliamua kulifunga duka. Mwendapole baada ya kufungwa duka alijikuta akishindwa kumalizia ujenzi wa nyumba yake.

**MASWALI**

(1) Ni kwa nini Mwendapole alishindwa kumalizia ujenzi wa nyumba yake?

(2) Ainisha makosa ambayo yanaweza kuwa ndiyo yamesababisha wakaguzi kufunga duka la Mwendapole.

(3) Ni mambo gani ya hatari ambayo yangeweza kujitokeza kama duka lisingefungwa?

## Kiambatanisho 2

## ILIHALI (MODULI 1; SURA 2)

### MAADILI YA MTOA DAWA

Faraja ni mtoa dawa katika Duka la Dawa Muhimu lijulikanalo kwa jina la Tegemeo lililoko mjini Kilosa. Kwa kuzingatia Kanuni za DLDM yeye ndiye anayeshughulikia mambo yote yanayohusiana na kutoa dawa kwa wateja. Faraja ni binti mkarimu sana kwa hiyo huwa anawasidia kuwapa wateja dawa wanayopendekeza wao na hata kama muda wake wa matumizi umekwisha huweza kubadilisha lebo ili wasibugudhiwe na polisi njiani.

Faraja hupenda kutengeneza nywele zake kwenye saluni ijulikanayo kwa jina la Tupendane ambako kuna rafiki yake aitwaye Asha. Anapokuwa anatengeneza nywele zake hupata fursa ya kupeana michapo na rafiki yake ambapo humhadithia jinsi anavyotoa huduma kwenye DLDM ikiwa ni pamoja na kutaja wagonjwa wenye magonjwa ya ngono na Ukimwi kutoka katika kitongoji anakoishi ambao hufika dukani kuomba huduma.

**MASWALI**

(1) Taja maadili ambayo Faraja aliyakiuka.
(2) Taja kanuni za uendeshaji wa DLDM alizokiuka Faraja.
(3) Ungepata nafasi ya kumshauri Faraja, ungemwambia azingatie nini kama mtoa dawa?

**Kimbatanisho 3**

**IGIZO (Moduli 1; Sura 1)**

**TARATIBU NA HATUA ZA UANZISHAJI WA DLDM**

(1) Waeleze washiriki kuwa sasa ni muda wa kufanya Igizo la taratibu za uanzishaji DLDM. Onyesha (Display) bango lenye maelekezo ya jinsi ya kufanyia igizo.

(2) Omba watu watano watakaojitolea kufanya igizo la taratibu za uanzishaji wa DLDM.

(3) Waeleze wachague kwa hiari majukumu yao. Kila mmoja achague nafasi moja kati ya:

a) Mwombaji wa DLDM
b) Afisa Mtendaji wa kijiji – VEO
c) Mganga wa zahanati/kituo cha Afya (Mkaguzi)
d) Afisa Mtendaji wa Kata (WEO)
e) Katibu wa DDTC – Mfamasia wa wilaya

(4) Toa maelekezo kwa waigizaji pasipo wengine kusikia

(i) Mwombaji
- Anaenda kuchukua fomu kwa Katibu wa DDTC
- Mwombaji anakaribishwa, kuamkiana na kutoa shida yake.
- Katibu anampa fomu na risiti ya malipo baada ya kupokea fedha (gharama ya fomu).

(ii) Mwombaji anarudi na fomu nyumbani na kuijaza.

(iii) Mwombaji anawasilisha fomu iliyojazwa kwa VEO

(iv) VEO – atahifadhi fomu ya maombi hadi siku ya kikao – ambapo itajadiliwa na kutolewa maoni na Kamati (Azungumze tu) – (Kamati ya Elimu, Afya na Ustawi wa Jamii).

(v) VEO atampelekea WEO fomu ya maombi ikiwa na mapendekekzo ya kijiji.

(vi) WEO – anawaomba wakaguzi (Mganga wa kituo) – wakakague eneo na kuweka mapendekezo na kuirejesha kwa WEO. Aidha, mwombaji anaelekezwa apeleke watoa dawa kwenye mafunzo ya DLDM na mmiliki pia kuhudhuria mafunzo ya umiliki

(vii) WEO – anawasilisha fomu ya maombi pamoja na mapendekezo kwa katibu wa DDTC na kurudi.

(viii) Katibu wa DDTC – anawasilisha maombi kwa kamati ya kitaalamu ya Dawa ya Wilaya (DDTC).

(ix) Kamati ya kitaalamu ya dawa inafanya kikao na inatoa maamuzi ya maombi ya mhusika kumpa kibali cha kufungua DDLM mwombaji baada ya kutimiza vigezo

(x) Katibu wa DDTC – anapeleka taarifa pia kwa RDTC na TFDA kwa ajili ya kuandaa kibali

(5) Waelekeze kila mmoja achukue nafasi kwa kuketi katika kiti kilicho kwenye bango lililoandikwa cheo kinachofanana na kile alichokichagua.

(6) Hakikisha Katibu wa DDTC anakuwa na fomu za maombi

(7) Ruhusu igizo lianze kwa kumtaka mwombaji kwenda kuchukua fomu toka kwa Katibu wa DDTC.

(8) Washiriki wengine waelekezwe kusikiliza na kuainisha mapungufu ya maeneo yanayohitaji kuboreshwa.

(9) Waigizaji wapewe nafasi ya kueleza uzoefu wao.

(10) Ruhusu maswali na majadiliano toka kwa washiriki wengine.

(11) Linganisha dhana ya igizo na mambo yaliyoko kwenye kitabu cha mafunzo kwa kutoa mifano.

(12) Hitimisha kwa maswali na majibu.

**Kiambatanisho 4**

**IGIZO DHIMA (MODULI 2; Sura 4)**

**UTOAJI WA DAWA ZA CHETI**

**Mahitaji**

(a) Washiriki
(b) Cheti cha dawa
(c) Dawa

**Maelezo**

Washiriki wanne watahusika katika nafasi mbili – mgonjwa na mtoa dawa. Washiriki watagawanyika katika sehemu mbili (A na B).

**Sehemu A – Utoaji wa dawa usiofuata hatua**

Mgonjwa anafika katika DLDM na cheti cha dawa. Mtoa dawa katika DLDM anapokea cheti na anafunga dawa kwenye bahasha bila kuuliza kama mwenye cheti ndiye anayeumwa. Anampa dawa mgonjwa na kumpa maelezo ya 2x3 (mbili kutwa mara tatu).

**Sehemu B – Utoji sahihi wa dawa**

Mgonjwa: anafika katika DLDM na kumpa cheti mtoa dawa.

Mtoa Dawa:

- Baada ya kupokea cheti anamsalimia mgonjwa na kumuuliza maswali kwa nia ya kuhakiki cheti.
- Anasoma cheti cha mgonjwa na kuelewa na kukitafsiri
- Anafunga dawa katika bahasha ambayo ina lebo ya dawa husika
- Anaweka kumbukumbu za dawa zilizotolewa
- Anampa dawa mgonjwa pamoja na maelezo sahihi na ushauri kama ifuatavyo:
    - o *Dawa hii inaitwa Aspirini, ni ya maumivu na kupunguza homa.*
    - o *anashauriwa kuimeza baada ya kuwa amekula na anywe maji mengi.*
    - o *Meza vidonge viwili kila baada ya saa nane.*
    - o *Je umeelewa nilivyo kuambia?*
    - o *Kama ndiyo waweza kusema ulivyoelewa?*)

**Swali**

1. Washiriki watofautishe waliyoyaona kati ya Sehemu **A** na **B**
2. Ni yupi alitoa dawa kwa usahihi na kwa nini?

**Kiambatanisho 5**

**ILIHALI (MODULI 3; Sura 4)**

**MAGONJWA YANAYOKEA MARA KWA MARA KATIKA JAMII**

Ni hivi karibuni Juma mwanafunzi wa shule ya msingi Mogani aligundua kuwa Samweli, ambaye ni mwanafunzi ambaye aliyehamia shuleni kwao akitokea Tukuyu, anakojoa mkojo mweupe kabisa tofauti na yeye na watoto wengine wa hapo shuleni ambao wote wamekuwa wakikojoa mkojo wa rangi ya kahawaia inayoelekea kuwa nyekundu.

Kila mmoja wao alimshangaa mwenzie. Juma, kwa ujasiri aliamua kutoa taarifa kwa mwalimu wa somo la afya na maarifa. Mwalimu alitoa taarifa hii kwa mganga wa kituo cha afya  cha karibu ambaye hakuchelewa kugundua tatizo hili la kijamii. Ilileweka kuwa karibu watoto wote katika eneo hili walikuwa wanakojoa mkojo kama ule wa Juma na wengine. Hakuna aliyefikiria kuwa hili lilkuwa ni tatizo kwani kila mmoja alikuwa hivyo na ilifikiliwa asiye kojoa mkojo wenye damu ndiye mwenye matatizo.

**Maswali**

(i) Ni tatizo gani lililokuwa linaikabili jamii?
(ii) Toa sababu za kuwepo kwa tatizo hilo
(iii) Taja tiba ya tatizo hilo
(iv) Taja kinga za kukabiliana na tatizo hilo

**Kiambatanisho 6**

**IGIZO FUPI (MODULI 4; SURA 2)**

**MAGONJWA YA KUJAMIIANA**

Bw. Hassan Mamboleo ametoka Sokoine Hospitali kutibiwa ugonjwa wa kutokwa na uchafu kwenye uume unaosababishwa na kujamiiana , ametibiwa na kuandikiwa dawa kadhaa mojawapo ni Doxycyline 100mg bid 7/7, amefika katika DLDM na umemuuzia dawa na kutoa maelekezo sahihi ya kutumia dawa hiyo.

**Kazi:**

Mpe elimu ya afya ili aweze kuepuka ugonjwa kumrudia na madhara ya magonjwa yatokanayo na kujamiiana.

## Kiambatanisho 7

## IGIZO FUPI (MODULI 4; SURA 3)

## UKIMWI

Kijiji cha Mdundo kuna chama cha watu waishio na virusi vya UKIMWI na UKIMWI.Watu wengi huwanyanyapaa ikiwa ni pamoja na vijana hasa wa shule ya Makumbusho kijijini hapo Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo amekuletea vijana ukiwafundisha juu ya Unyanyapaa na mambo teule wanayoweza kuyakwepa ,vijana hao ndio watakaofundisha wanafunzi wenzao.

Wakati wewe, Mwendapole Mtoa Dawa ukiwaelezea mmoja wa vijana hao akakueleza anaishi na VVU.

**Shughuli**

- Toa somo la Unyanyapaa kwa vijana wa shule wawili ili wao nao wakafundishe wenzao kama ulivyofundishwa.
- Onyesha kutomnyanyapaa mmoja wa vijana hao.

**Kiambatanisho 8**

**ILIHALI (MODULI 5; Sura 2)**

**ELIMU YA AFYA**

Bwana Juma Pesambili amefika katika DLDM –Mpanda amefika kutoka Kituo cha Afya, anasumbuliwa na kifua kikali, amefika na cheti cha mganga amabcho kimeandikwa dawa ya Amoxycillin Kapsuli 500mg kila baada saa 8 kwa siku 5, lakini Bw Juma Pesambili anataka vidonge vya siku mbili tu ana hakika atakuwa amepona maana mara nyingi amefanya hivyo na kufanikiwa.

**Kazi:**

1. Je umegundua tatizo gani kuhusu matumizi sahihi ya dawa kwa Bw. Pesambili
2. Toa elimu kwa Bw. Pesambili itakayosaidia kurekebisha tatizo hili kwa kuzingatia mafunzo uliyopata kuhusu matumizi sahihi ya dawa (Zoezi hili lifanyike katika vikundi).

## Kiambatanisho 9

## IGIZO FUPI (MODULI 5; SURA 3)

## USHAURI NASAHA

Bibi Chiwango amefika katika DLDM – Ligula anajisikia mwili mzima unamuuma na kichwa kinamuuma pia. Anahitaji vidonge vya Quinine .Bi Chiwango hana cheti cha mganga maana siku za nyuma alitumia hivyo na kupata nafuu kabisa.

**Kazi:**

1. Je umegundua kwamba Bi Chiwango ana tatizo gani ya kuongelea?
2. Je ni kasoro zipi utakazomuelezea ili aweze kuamua kwa kutumia dawa sahihi?
3. Mpe ushauri nasaha kumsaidia kuamua kutumia dawa inayofaa.

## Kiambatanisho 10

## ILIHALI (MODULI 5)

## MBINU ZA MAWASILIANO NA UTOAJI SAHIHI WA DAWA

Ndg. Rashidi anaingia katika duka la dawa na anamkuta Ndg. Madaraka muuza dawa. Anapofika dukani, anamsalimia Ndg. Madaraka ambaye anaitikia akiwa anaendela na shughuli zake za kupanga dawa katika shelfu bila hata kumuangalia. Ndg. Rashidi anaendela kujieleza tatazo alilonalo kwa lengo la kuuziwa dawa, lakini anajibiwa na Ndg. Madaraka kuwa hakuna dawa huku akiendelea kupanga dawa bila hata kuonyesha kumjali. Rashidi naye anaamua kutoka dukani huku analalamika kuwa hukupewa huduma nzuri.

Rashidi anakwenda kwenye duka jingine la ndugu Akilimali na mambo yanakuwa hivi:

| | |
|---|---|
| Ndg. Rashidi | Anaingia dukani kwa Ndg. Akilimali. |
| Ndg. Akilimali | Anamkaribisha na **kumuonyesha kwa mkono** sehemu ya kukaa wakati akisubiri kuhudumiwa. |
| Ndg. Akilimali | **Anamuuliza** Rashid shida iliyo mleta huku wakiangaliana **ana kwa ana**.<br>Pindi zamu ya ilipofika, |
| Ndg. Rashid | Anajieleza kuwa anapata maumivu ya tumbo kwa muda wa siku mbili |
| Ndg. Akilimali | Anamsikiliza kwa makini, huku akionyesha ishara ya kuelewa kwa kichwa. Pia anamuuliza kama maumivu ya tumbo yanaamabatana na kuharisha. |
| Ndg. Rashidi | Anajibu kwa kusema ”ndiyo” |
| Ndg. Akilimali | Anamwelewesha kuhusu dawa anazoweza kutumia kwa ajiri ya tatizo alilonalo na umuhimu wa kwenda kituo cha tiba kwa uchunguzi zaidi |
| Ndg. Rashidi | Ananunua dawa na anashukuru kwa kusema, “nimeridhishwa na huduma yako ahasante sana na anaondoka”. |

**Maswali**

1. **Waulize** washiriki wameona na kujifunza nini juu ya huduma kati ya Duka la Ndg. Hamisi na Akilimali?
2. **Waulize** kama wana weza kuanisha sehemu ambapo lugha za ishara zimetumika katika maigizo haya.
3. Waeleze washiriki faida ya kutumia lugha za ishara na mazungumzo katika kufiksha ujumbe

## Kiambatanisho 11

## ILHALI (MODULI YA 2 NA 5)

## MBINU ZA MAWASILIANO NA UTOAJI SAHIHI WA DAWA

Bwana Bulobazi ni mzee wa makamo kutoka Kata ya Majimoto. Ni mfugaji wa ngombe hushinda nyikani asubuhi hadi jioni. Kazi hii huifanya na mtoto wake aitwaye Kalitopia mwenye umri wa miaka 12. Siku moja wakiwa malishoni, Kalitopia alijikwaa na kuanguka ambapo aliumia sana kwenye mguu wa kushoto na damu nyingi zilitoka. Alimmfunga na majani kuzuia damu kisha bila kuchelewa Bwana Bulobazi akambeba mtoto wake na kumpeleka kwenye duka la dawa la dawa baridi la Nomi. Alimkuta muuza dawa aitwaye Kalitunga.

Kufika katika duka la Nomi, mambo yanaenda hivi kati ya Bulobazi na Kalitunga:

Bulobazi: “Nipatie vidonge vya Pen V haraka iiwezavyo

Kalitunga: ”kidonge kimoja shilingi 50 unataka vingapi” (huku akiongea na simu yake ya mkononi)

Bulobazi: ”nipatie sita, mhh hapana nipe vitatu vitatosha”

Kalitunga: bila kuuliza zaidi na huku akiongea na simu anachukua kopo na kwa kutumia vidole vyake anachukua vidonge vitatu na kumfungia kwenye kipande cha gazeti. Wakati anafunga kidonge kimoja kikaanguka sakafuni na akakichukua na kukirudishia kwenye kopo. Akachukua zile dawa alizofunga kwenye gazeti na kumpatia kalitunga bila kumwambia chochote.

Bulobazi: baada ya kulipa, anaaga na kwenda nyumbani kwake ambapo anasaga vile vidonge na kumwekea kwenye kidonda mtoto wake Kalitopia.

**Maswali:**

(i) Je ni Kalitunga alifanya makosa gani katika utoaji wa dawa
(ii) Je ndugu Kalitunga alitakiwa kuchukua hatua gani katika kumhudumia Bulobazi
(iii) Je kuna hatari gani za kutumia dawa kama alivyofanya Bulobazi